

**UCHUNGUZI WA VIPENGELE TEULE VYA FANI KATIKA**

***MASHETANI WA ALEPO***

**NA**

**NGUNYI SAMUEL KANG'ERI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA**

**NAIROBI.**

**2017**

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada za uzamili.

SAHIHI\_\_\_\_\_

TAREHE\_\_\_\_\_

**Ngunyi Samuel Kang'eri**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

SAHIHI\_\_\_\_\_

TAREHE\_\_\_\_\_

**Profesa Mwenda Mbatiah**

SAHIHI\_\_\_\_\_

TAREHE\_\_\_\_\_

**Daktari Evans M. Mbuthia**

## **TABARUKU**

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu Bw. Charles Ngunyi na Bi. Agatha Wanjiru walionilea na kunisomesha na kunifanya niwe na kiu ya masomo ili niweze kufaulu maishani.

## **SHUKRANI**

Safari hii imekuwa ya pandashuka nyingi iliyohitaji uvumilivu na makini nyingi ili kuhakikisha tumefika mwisho wake. Imefanikishwa na kufikia kikomo kutokana na usaidizi wa watu wengi ambao sina budi kuwashukuru ingawa sitaweza kuwataja wote.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote ambao walichangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya nzuri na uwezo wa kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili.

Ninatoa shukrani maalum kwa wasimamizi wangu, Prof. Mwenda Mbatiah na Dkt. Evans Mbuthia kwa ushauri wao wa kitaaluma na kwa kuhakikisha kuwa kazi hii imetimia. Sina cha kuwapa ila kuwaombea Mungu awazidishie afya na maarifa. Mungu awabariki sana. Shukrani nyingi ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa ushauri walionipa na uliochangia katika kufikia malengo yangu. Shukrani maalum kwa Prof. M. H. Abdulaziz, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Rayya Timammy, Prof. J. Habwe, Prof Iribi Mwangi aliyekuwa akitushughulikia na kuona kwamba masilahi yetu yanatekelezwa. Wengine ni Dkt. Tom Olali, Dkt. A. Mukhwana, Dkt. A. Buregeya, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. H. Mwaliwa, Dkt. B. Mungania na Dkt. P. Jerono. Mungu awabariki sana. Ninawashukuru wazazi wangu, Bw. Charles Ngunyi na Bi. Agatha Wanjiru walionizaa na kunionyesha milango ya darasa. Vilevile ninawapa shukrani nyingi kwa kunifadhili kwa pesa za karo na pia za matumizi yangu wakati wa masomo yangu.

Shukrani nyingine ziwaendee wanafunzi wenzangu tuliosafiri katika chombo kimoja na kuhakikisha kuwa tumefika mwisho wa safari licha ya vizingiti kadhaa njiani. Nao ni Ngulamu Mwaviro, Edwin Muna, Albert Otwera, Joshua Anusu, Zipporah Kitiku, Lilian Chacha na Purity Kolongei.

Siwezi kusahau Tume ya Kuajiri Walimu (T.S.C) kwa kunipa likizo ya miaka miwili. Mwisho ningependa kumshukuru Njeri kwa kupiga taipu kazi hii na kuhakikisha kuwa imekamilika katika wakati unaofaa. Mungu awabariki nyote!

## **IKISIRI**

Tasnifu hii imeshughulikia uchunguzi wa vipengele teule vya fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha, usimulizi na maudhui kwa kuangalia jinsi mwandishi alivyovitumia katika kufanikisha *Mashetani wa Alepo*. Maarifa yetu ya kitaaluma yalijikita kwenye nadharia ya umuundo na uhalisajabu. Madhumuni ya utafiti huu yaliikuwa kuchanganua vipengele mahsusini vya fani na pia kuchunguza iwapo vinabainisha riwaya hii kama riwaya ya kimajaribio. Utafiti huu pia ulichunguza kwa nini riwaya hii inaanishika kama riwaya ya kimajaribio. Maswali matatu yaliyoongoza utafiti huu ni fani imetumiwaje kuendeleza ujumbe katika *Mashetani wa Alepo*? Je ni maudhui yapi yaliyowasilishwa katika *Mashetani wa Alepo*? Na pia kwa nini *Mashetani wa Alepo* inaanishika kama riwaya ya kimajaribio? Matokeo ya utafiti wetu yamethibitisha kuwa vipengele vya fani vilitumiwa kwa ufundu wa hali ya juu jambo ambalo lilichangia mwandishi kuendeleza ujumbe wake kwa njia inayoleweka kwa urahisi. Pia fani imetumiwa kutia ladha na hivyo kumpatia msomaji msukumo wa kusoma riwaya hii. Maudhui tuliyoyashughulikia yametuwezesha kumulika uozo wa jamii ambao hutendeka ulimwenguni. Fani pia imetuwezesha kung'amua kwamba, riwaya hii ni ya kimajaribio.

## **YALIYOMO**

UNGAMO.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI .....	vi
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	4
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	5
1.4 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .....	5
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	6
1.7 Msingi wa Kinadharia.....	7
1.7.1 Uhaliisiajabu .....	7
1.7.2 Nadharia ya Umuundo .....	9
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .....	12
1.9 Njia za Utafiti.....	14
1.10 Hitimisho.....	15
<b>SURA YA PILI: FANI KATIKA RIWAYA YA MASHETANI WA ALEPO .....</b>	<b>16</b>
2.1 Utangulizi.....	16
2.2 Mandhari .....	16
2.2.1 Chumba cha kulala cha Megido.....	17
2.2.2 Msitu wa Alepo .....	19

2.2.3 Mandhari ya Maabara ya Eksirei .....	21
2.2.4 Mandhari ya Uwanja wa ndege wa Alepo .....	23
2.2.5 Mandhari ya Mahakamani .....	24
2.2.6 Mandhari ya Ndege.....	24
2.3 Matumizi ya Lughya na Mbinu Nyinginezo.....	25
2.3.1 Takrirri .....	25
2.3.2 Tashbihi .....	27
2.3.3 Tanakali Sauti.....	28
2.3.4 Methali na Misemo .....	29
2.3.5 Kuchanganya Msimbo na Kuhamisha Msimbo .....	31
2.3.6 Chuku.....	33
2.3.7 Ukiushi wa Kisintaksia .....	34
2.3.8 Tashihisi .....	34
2.3.9 Maswali ya Balagha.....	35
2.3.10 Nyimbo .....	35
2.3.11 Taswira .....	36
2.3.12 Dayalojia.....	42
2.3.13 Ukiushi wa Kimsamiati.....	42
2.3.14 Matumizi ya Maneno ya Kigeni .....	44
2.4 Usimulizi.....	44
2.5 Hitimisho.....	53
<b>SURA YA TATU: FANI INAVYOIMARISHA MAUDHUI KATIKA MASHETANI WA ALEPO .....</b>	<b>54</b>
3.1 Utangulizi.....	54

<b>3.2 Jinsi Fani Inavyoimariswa Maudhui Katika <i>Mashetani wa Alepo</i> .....</b>	<b>54</b>
3.2.1 Maudhui ya Kidini .....	54
3.2.2 Uchafuzi wa Mazingira.....	55
3.2.3 Athari Mbaya za Teknolojia.....	56
3.2.4 Mauaji ya Kimbari .....	57
3.2.5 Dawa za Kulevyा .....	58
3.2.6 Ndoa.....	58
3.2.7 Ufisadi.....	58
3.2.8 Biashara Haramu.....	59
3.2.9 Siasa na Uchumi Katika Jamii .....	60
3.3 Mandhari Yanavyoimariswa Maudhui kwa Ujumla .....	62
3.4 Nafasi ya Nyimbo katika Uimarishaji wa Maudhui .....	63
3.5 Nafasi ya Methali Katika Uimarishaji wa Maudhui .....	64
3.6 Nafasi ya Dayalojia Katika Uimarishaji wa Maudhui .....	66
3.7 Hitimisho.....	67
 <b>SURA YA NNE: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	 <b>68</b>
4.1 Utangulizi.....	68
4.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	68
4.3 Hitimisho.....	70
4.4 Mapendeleko .....	73
 <b>MAREJELEO .....</b>	 <b>74</b>

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Utangulizi

Kulingana na Wamitila (2008) fani ni dhana itumiwayo kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Wahakiki wa kazi za kifasihi aghalabu hupenda kuonyesha tofauti iliyoko kati ya fani na yaliyomo au maudhui. Pili ni vyema kukumbuka kwamba, dhana hizi mbili huchangizana. Mawazo ya Wamitila yanaelekea kushahibiana na ya Mbatiah (2001) anayefafanua fani kama jumla ya vipengele vyta kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubeba ujumbe na maana mahsus.

Katika utafiti wetu tutashughulikia vipengele mahsus vyta fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi jinsi vinavyochangia uendelezaji wa ujumbe katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo* iliyoandikwa na Tom Olali (2015). Mwandishi wa riwaya tunayoishughulikia ameandika riwaya zingine ambazo ni *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* (2002). Hata hivyo, tumejikita katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo*.

Riwaya hii inaweza kuorodheshwa katika tapo la riwaya za kimajaribio kwa sababu inakiuka kabisa kaida za utungaji na muundo wa riwaya uliozoleka na pia inahusisha mtindo wa kishairi. Vilevile, msuko na wahusika vimo katika hali ambayo si ya kawaida. Kwa mfano, wahusika wanaweza kuwa na nafsi mbili. Riwaya hii inaangazia mapigano ya kimbari mionganoni mwa jamii mbili nchini Alepo ambazo ni za Wanyakwelekere na Wamaya yanayopelekea mauaji makubwa.

Riwaya hii imeangazia masuala ibuka yanayotokea katika jamii zetu kama: utawala wa kimabavu, ufisadi, vita vya kikabila, biashara haramu ya mihadarati na ukatili dhidi ya haki za binadamu. Vilevile imemulika uozo wa kimaadili na jinsi taifa linavyonadiwa kwa wageni ambao wanaligeuza kuwa jaa la kurundika dawa za kulevya.

Katika *Mashetani wa Alepo*, mwandishi ametumia vipengele mbalimbali vya kimitindo ambavyo vimechangia uchangamano wa riwaya hii kwa mfano, amesimulia hadithi kadha ndani ya hadithi kuu. Aghalabu hadithi hizo ndogo ni jazanda za mambo fulani katika hadithi nzima. Kwa hivyo, ni vyema kusitiza kuwa hadithi hizi ndani ya hadithi kuu zimechangia kuendeleza hadithi kuu.

Matumizi ya hadithi mbalimbali ndani ya moja yamesababisha utumizi wa wahusika wengi katika riwaya hii. Katika riwaya hii pia kuna matumizi ya mbinu rejeshi, upana mkubwa wa mandhari, lugha isiyo ya kawaida ambayo ni thibitisho kamili kuwa riwaya hii ni changamano.

*Mashetani wa Alepo* vilevile inaweza kutazamwa kama riwaya mpya kwa kuwa matukio na vipengele vingine katika riwaya hii vinaibainisha kama riwaya mpya. Kwa mfano, riwaya hii imechanganya lugha ya msimulizi na wahusika, kuna uakifishi usio wa kawaida, na wahusika wasio na sifa zinazowabainisha waziwazi. Aidha, riwaya hii imechanganya mbinu za kisaikolojia, kimaajabu na kiuhalisi.

Sifa za riwaya hii ni dhihirisho kamili kuwa inaweza kuangaziwa katika matapo mbalimbali ya riwaya kama nilivyoleza hapo mbeleni. Jambo hili limetupatia motisha kuchunguza jinsi fani inavyoendeleza ujumbe katika kufanikisha kazi nzima

ya riwaya hii. Maudhui ni kipengele muhimu katika uandishi wowote wa kisanaa maanake hutuwezesha kung'amua mawazo ya mwandishi katika uandishi wake.

Maudhui ndicho kiini kikuu cha kazi yoyote ya fasihi kwa kuwa mwandishi anapoianidika kazi yake, lazima awe na lengo ambalo lilimsukuma kuandika kazi yenye. Vile vile lazima awe na ujumbe ambao anataka kuwasilisha kwa hadhira lengwa. Fani na maudhui ni vipengele ambavyo havistahili kutenganishwa kamwe kwa kuwa dhana hizi mbili huchangizana.

Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila kutumia lugha. Lugha hiyo huwa na sifa fulani. Kwa mfano, huwa ina vikolezo au vitia ladha fulani, inasheheni au kujaza mbinu za kila aina. Haiwezekani kwa mwandishi kuiwasilisha dhamira yake au maudhui yake bila ya kuitegemea fani. Ikiwa mwandishi atataka kuwasiliana na msomaji wake vyema pamoja kumshawishi na kumwathiri ipasavyo, lazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kuwa lugha yake ina uwezo wa kuwasilisha ujumbe huo. Uhusiano wa fani na maudhui ni muhimu sana na ni wa kutegemeana; ni kama upande mmoja wa sarafu na mwingine.

Wamitila (2002) akielezea kuhusu uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui anasema kwamba, tuchukue mfano wa upishi ambapo mtu anayetaka kusonga ugali anahitaji maji, sufuria, unga na mwiko. Ugali hauwezi kupatikana bila ya kuwako na vitu hivyo. Anasema kwamba dhamira na maudhui ni kama ugali ilhali vitu vingine ni fani. Kutokana na madai haya tunaweza kusema kwamba, kufaulu au kufanikiwa kwa msanii kuendeleza ujumbe kwa ukamilifu kutategemea jinsi alivyoshirikisha fani katika kazi yake.

Ninakubaliana na maoni ya Wamitila kuwa ili mwandishi afanikishe uendelezaji wa maudhui yake, lazima ahusishe fani. Kufanikiwa kwa mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* katika uendelezaji wa maudhui kumetegemea jinsi alivyoshirikisha fani katika kazi yake.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Mwandishi yejote wa kazi ya fasihi ana uhuru wa kutumia vipengele vyta fani jinsi atakavyo ili kukidhi mahitaji ya kazi yake. Jambo hili hutofautisha kazi ya msanii mmoja na mwingine. Vilevile tofauti za kitanzu huwafanya waandishi watumie mitindo inayofaa katika uandishi wao kwa kutegemea utanzu unaohusika.

Mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* ametumia vipengele mbalimbali vyta fani kuendeleza ujumbe wake. Ametumia mandhari ya aina tofauti tofauti kwa mfano msitu wa Alepo, mito, majengo ya kisasa yenye maabara, milima ya taka na pia ametumia uwanja wa ndege. Vilevile ametumia wahusika wa makundi na aina tofauti tofauti kama vile viongozi wa vikundi haramu, wanasiasa miiongoni mwa wahusika wengine. Aidha ametumia hadithi mbalimbali katika usimulizi wake.

Ufundu uliotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa mnato. Vilevile unampatia msomaji mvuto fulani anapoisoma kazi yenye. Fani si njia horomo inayotumika kuendeleza maudhui. Uteuzi wa kiufundi wa fani unaweza kuimarisha uwasilishaji wa maudhui kama tulivyothibitisha katika utafiti huu.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

- i. Kuchanganua vipengele mahsusи vya fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi na pia kuchunguza iwapo vinabainisha *Mashetani wa Alepo* kama riwaya ya kimajaribio.
- ii. Kuchanganua maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo*.
- iii. Kuchunguza kwa nini riwaya ya *Mashetani wa Alepo* inaainishika kama riwaya ya kimajaribio.

### **1.4 Maswali ya Utafiti**

- i) Fani imetumiwaje kuendeleza ujumbe katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo*?
- ii) Je, ni maudhui yapi yaliyowasilishwa katika *Mashetani wa Alepo*?
- iii) Kwa nini *Mashetani wa Alepo* inaainishika kama riwaya ya kimajaribio?

### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Sababu ya kwanza ya kuchagua mada hii ni kuwa riwaya ya *Mashetani wa Alepo* haijawahi kufanyiwa utafiti wa kiakademia hapo awali. Jambo hili limetupatia motisha kuchagua mada hii. Tunaamini utafiti huu utasaidia katika uelewekaji wa riwaya hii. Vilevile, utafiti huu utaongezea maarifa kuhusu uhakiki wa riwaya za kiamajaribio.

Pili, baada ya kusoma *Mashetani wa Alepo*, tumeng'amuа kwamba, kazi hii haijatumia mtindo uliozoleka wa uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Kwa mfano kuna matumizi mengi ya mbinu rejeshi katika msuko wa riwaya hii. Vilevile mwandishi amewatumia wahusika wasio wa kawaida. Vilevile kuna matukio mengi

ya kuduwaza na kuogofya katika riwaya hii. Kutohana na ung'amuzi huu tuliamua kuihakiki kazi hii kifani ili tuchunguze jinsi mwandishi alivyotumia vipengele vyta fani kuendeleza ujumbe wake. Utafiti huu utachangia pakubwa katika uelewekaji wa riwaya za kiuhalisiajabu na za kimajaribio. Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha watafiti wa baadaye kuhakiki tanzu nyingine za fasihi zenyenye mwelekeo wa kiuhalisiajabu. Tatu, tuliteua mada hii kwa nia ya kuibua mtazamo mpya wa kuihakiki riwaya hii.

### **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu utashughulikia riwaya moja pekee ambayo ni *Mashetani wa Alepo*. Katika riwaya hii, tutachanganua vipengele mahsusini vyta fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi kwa kuchunguza jinsi vilivyotumiwa kuendeleza ujumbe katika riwaya hii.

Tumeteua vipengele hivi kwa kuwa vimechukua nafasi kubwa katika riwaya hii. Vipengele hivi vimechangia pakubwa katika kuipa kazi hii muundo na maana mahsusini kwa sababu mwandishi amevitumia kama malighafi muhimu katika kuendeleza na kujenga kazi yake. Kwa hivyo, utafiti huu hauna budi kuvichunguza. Vilevile tulivateua kwa kuwa vinahusiana na kujengana katika uendelezaji wa maudhui katika kazi hii. Utafiti huu utaongozwa na nadharia za umuundo na uhalisiajabu ambazo tutazitumia kuonyesha jinsi vipengele mbalimbali vyta fani vilivyotumiwa kuendeleza ujumbe katika kazi hii.

## **1.7 Msingi wa Kinadharia**

Nadharia ambazo tutatumia katika utafiti wetu ni za Umuundo na Uhalsiajabu.

Tutatumia nadharia hizi mbili katika uhakiki wetu ili kufikia madhumuni yetu tuliyoyataja hapo mwanzoni.

Kulingana na Mbatiah (2001),

Nadharia ni mfumo wa kimawazo wenye teneti au kanuni mahsusini, unaotoa mwongozo wa jinsi ya kushughulikia na kuhakiki fasihi. Mwongozo huo unajumlisha vigezo, taratibu na mikakati ya kuainisha, kufafanulia na kuchambulia tungo za kifasihi. Misingi ya nadharia katika fasihi iliwekwa na wanafasihi wa kipindi cha Urasimi.  
(uk.61-65).

Ninakubaliana na mawazo ya Mbatiah kuwa ili mhakiki yezote aweze kuhakiki kazi fulani ya kisanaa, lazima awe na mwongozo unaomtawala katika kushughulikia kazi yenye. Katika utafiti wetu, hatuna budi kutumia nadharia nilizozitaja ili zitupatie mwongozo mwafaka wa kuhakiki *Mashetani wa Alepo*.

### **1.7.1 Uhalsiajabu**

Kwa mujibu wa maelezo ya Zamora (1995) nadharia ya uhalsiajabu ilianza mnamo mwaka wa 1925. Mwanzilishi wake alikuwa mhakiki wa sanaa wa Kijerumani aliyeitwa Franz Roh. Dhana ya Roh *nach-expressionismus, magischer Realismus* ikitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili inaashiria hali ya uajabu au umazingaombwe. Uhalsiajabu unaelezee miujiza iliyomo kwenye uyakinifu wa kila siku.

Maelezo ya Roh yatatufaa katika uhakiki wetu kwa kuwa riwaya tunayoishughulikia ina matukio mengi yaliyosawiriwa kwa njia ya kimazingaombwe ingawa yanafanyika katika ulimwengu wetu wa kila siku.

Mbatiah (2001), anafafanua uhalisiajabu hivi:

Istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Uhalisia wa kimaajabu huhushishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka Bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia. (uk.60).

Kulingana na maelezo ya Mbatiah, nadharia ya uhalisiajabu itakuwa na umuhimu kwetu kwani mambo mengi katika riwaya hii ni ya kiajabu ajabu lakini yameelezewa kwa kuiga mtindo wa kiuhalisia. Yaani yanaelezewa kana kwamba ni mambo ya kawaida. Ingawa mambo hayo yameelezewa kwa njia ya kiajabu, hutokea katika maisha ya kawaida katika jamii zetu.

Kulingana na Wamitila (2003),

Dhana ya uhalisiajabu huhushishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu. Sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika. (uk.274)

Maoni haya yanashabihiana na yale ya Mbatiah ambaye tumetangulia kumnukuu. Maoni yake kuhusu uhalisiajabu yatatupatia mwongozo wa kutumia nadharia hii katika utafiti wetu kwa kuwa mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* ametumia umazingaombwe kuonyesha kuwa matukio husika hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zetu. Ni nadharia ambayo inaelezea ukiukaji wa sifa za uhalisia kama zilivyozolewa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini.

Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa kama ya kawaida. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida (Cooper, 1998). Hali za kushangaza na kuogofya huwasilishwa kama kwamba ni za kawaida. Katika uhalisiajabu ndoto na uhalisi vinachanganywa. Pamoja na haya, mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, maanake ni kuwa wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile ya jamii, nchi au bara moja.

Katika *Mashetani wa Alepo* kuna hali za kuduwaza na kuogofya kwa mfano pale Megido ameketi kisha anaiona maiti yake ikiwa imelala kitandani, kilichorembeshwa na ngozi ya ngwena na yakuti samawi. Vilevile kuna matukio mengine mengi ya kushangaza na kuogofya katika riwaya hii na ndipo tukaona kwamba, nadharia ya uhalisiajabu itatusaidia katika uhakiki wetu ili kupata matokeo mwafaka.

### **1.7.2 Nadharia ya Umuundo**

Nadharia ya umuundo ilianza Urusi na ilianza kutumiwa katika uhakiki wa kazi za kifasihi mnamo mwaka wa 1920. Wataalamu kama vile Scholes na Fokkema (1974) wanadai kuwa asili ya nadharia ya umuundo ni nchini Ufaransa, ambapo ilichipuka katika miaka ya Hamsini na Sitini, kufuatia utafiti wa mwanaanthropolojia Claude Levi – Strauss aliyechanganya visaasili katika misingi ya isimu miundo iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure. Wanaisimu wa shule ya Prague kama Roman Jakobson, Borris Tomaserky, Nikolai Trubetzkoy na wengine walitoa mchango muhimu katika kuchipuka kwa umuundo. Urasimu na umuundo hutumiwa katika uhakiki wa kifani.

Hata hivyo, kuna wataalamu wengine kama vile Wamitila, Mbatiah na wengine ambao ni wahakiki kutoka Afrika wanaoelezea chimbuko la nadharia hii. Wamitila (2003) anasema kwamba, umuundo ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya uhakiki ambayo inachunguza kaida zilizopo katika uundwaji wa kazi fulani. Vilevile anaendelea kusema kuwa ukuaji wa nadharia hii unahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa.

Wamitila (2002) anaunga mkono mawazo ya Scholes (1974) anaposema kwamba, nadharia ya umuundo inahusishwa na wanaisimu wa shule ya Prague. Prague ulikuwa ni mji ambao wanaisimu walitorokea baada ya kupigwa marufuku huko nchini Urusi.

Nadharia ya umuundo iliathiriwa pakubwa na mawazo ya mwanaisimu wa Ki-Swizi, Ferdinand de Saussure ambaye alijikita katika lugha. Yeye alikuwa na mawazo tofauti kuhusu uchanganuzi wa lugha. Kabla mawazo ya mtaalamu huyu kuanza kutumiwa katika uchanganuzi wa lugha, lugha ilikuwa ikiangaliwa kama mkusanyiko wa viungo tofauti tofauti.

Mwanaisimu huyu alitofautisha kati ya matendo ya kiusemi (*parole*) na mfumo mpana wa lugha (*langue*). Tamko lolote huwa na maana tu ikiwa litaangaliwa katika upana wa msimbo wa lugha ya kijumla inayotumiwa na wanajamii. Kwa mtazamo huu fasihi inakua au inaangaliwa kama njia fulani ya utumiaji na usanifu wa lugha ambayo inaweza kuitwa lahaja ya kiuamilifu.

Mwanaisimu huyu alipendekeza uchanganuzi wa lugha kisinkronia ambao ni uchanganuzi wa lugha katika kipindi maalum. Mkabala huu ni tofauti na ule wa

kidaikronia ambao hutumika kuichanganua lugha kihistoria. Vilevile alibuni dhana za *langage*, *langue na parole*. Anaieleza dhana hii ya *langage* kama mfumo dhahania wa lugha ambao kila mwanadamu asiye na upungufu wa kusema huwa nao akilini mwake na humwongoza katika matumizi ya lugha. Dhana hii ya langage husimamia lugha zote na kwa hivyo tunaweza kuchukulia langage kama fasihi zote za kilimwengu.

Dhana ya *langue* huchukuliwa kama mfumo dhahania wa lugha fulani unaotumiwa na jamii fulani. Lugha kwa hivyo inaweza kuchukuliwa kama mfumo changamano ambao ndani yake kuna mifumo tofauti kwa mfano sintaksia, semantiki, na fonolojia mionganoni mwa mifumo mingine. Mifumo hii huwa na uhusiano na pia hukamilishana kama ilivyo katika vipengele vya fani na maudhui katika kazi za kifasihi kwa mfano riwaya ina viambajengo vya wahusika, msuko na mandhari mionganoni mwa vingine katika kuunda mfumo mmoja wa yaliyomo. Wazo hili limetokana na mawazo ya Ferdinand de Saussure ya kupinga kuchanganua lugha kwa kuangalia kiungo kimoja bila kuhusisha viungo mbalimbali. Wazo hili ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa tutaangazia vipengele mahsusisi vya fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi na jinsi vinavyohusiana katika kuendeleza ujumbe wa mwandishi katika utanzu wa fasihi tunaoushughulikia.

Kutokana na mawazo ya de Saussure fasihi inastahili kuchanganuliwa kama muundo mmoja ambao umejengwa kwa viambajengo tofauti tofauti vinavyohusiana au kuathiriana kuunda kitu kizima. Katika kazi yetu tutachunguza jinsi vipengele mahsusisi vya fani yaani mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi vinavyochangia uendelezaji wa ujumbe katika kuunda kazi nzima ya *Mashetani wa Alepo*.

Wamitila (2002) anasema kwamba, mwelekeo wa uhakiki wa kimuundo ni ufanuzi wa kazi za kifasihi bali sio kuzifasiri kazi hizo. Kimsingi uhakiki wa aina hii unajihuisha na kuangalia sehemu mbalimbali za kazi ya fasihi au viwango mbalimbali na kuonyesha jinsi vinavyounda muundo mzima. Wazo hili ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa tunanua kuangalia jinsi viambajengo mahsusini vyatia riwaya vinavyoshirikiana kuendeleza ujumbe wa mwandishi katika kazi husika. (uk.177).

### **1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Magaju (2004) katika tasnifu yake anatafitia riwaya ya *Babu Alipofufuka* ya S. A. Mohamed na *Bina–Adamu* ya K. W. Wamitila akitumia nadharia ya uhalisajabu. Uhakiki huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa kuwa ulituongezea maarifa kuhusu uchanganuzi wa riwaya za kimajaribio pia kuhusu jinsi nadharia ya uhalisajabu inavyotumiwa kuhakiki kazi za kitaaluma.

Olali (2010) alihakiki riwaya ya *Babu Alipofufuka* kwa anwani “Muundo (structure) na Dhidi-Muundo (Anti-structure) katika riwaya mpya ya *Babu Alipofufuka*” Katika utafiti huu anabainisha udhidi-muundo katika matumizi ya mbinu za uhalisajabu kwa mfano jinsi inavyodhahirika nyumbani mwa K. katika Limonsin na anapokuwa Neo-Casino. Anadhihirisha kuwa, muundo na mtindo katika riwaya za kimajaribio hutofautiana kwa kiwango kikubwa na kazi za kiuhalisia. Utafiti huu ulikuwa na umuhimu kwetu kwa kuwa ulituongezea maarifa kuhusu uhakiki wa riwaya za kimajaribio.

Bakari (2011) katika tasnifu yake ya uzamili alitafiti kuhusu “Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka, Bina-Adamu!* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda*”. Mtafiti huyu alibainisha vipengele mbalimbali vya kiuhalisiajabu. Vilevile alionyesha jinsi waandishi wa riwaya hizi wanavyotumia mtindo wa uhalisiajabu ili kueleza matatizo yanayoukumba ulimwengu wa sasa. Utafiti wa Bakari ulitufaa sana katika kuainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya tulioishughulikia. Mtafiti huyu alishughulikia maudhui katika riwaya mbili na hadithi fupi, lakini utafiti wetu umehusu uchunguzi wa vipengele teule vya fani, amavyo ni; mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi.

Tambasi (2011) katika tasnifu yake ya uzamili alihakiki fani akitumia nadharia ya umuundo. Kazi yake itatufaa katika utafiti wetu kwa kuwa itatuongezea maarifa kuhusu fani za kifashi. Kazi yake inatofautiana na yetu kwa kuwa yeye alihakiki utenzi wa *Tambuka* ilhali sisi tunahakiki riwaya ya kimajaribio.

Mugwika (2012) katika tasnifu ya uzamili, alitafiti “Dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*”. Utafiti huu ulichunguza uchimuzi katika kiwango cha wahusika na cha matumizi ya lugha kwa mtazamo wa nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Riwaya hii ya *Mafamba* inashahibiana na riwaya tunayoishughulikia ya *Mashetani wa Alepo* kwa kuwa zinakiuka kaida za uandishi wa kawaida. Utafiti huu ulitufaa sana katika utafiti wetu kwa kuwa ulituongezea maarifa kuhusu jinsi ya kuhakiki riwaya ya kimajaribio. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa kuwa sisi tulitafiti vipengele teule vya fani na jinsi vinavyoendeaza ujumbe katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo* kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu

na umuundo ilhali Mugwika alishughulikia dhana ya uchimuzi akitumia urasimu wa Kirusi.

Barasa (2013) katika tasnifu yake ya uzamili alitafiti kuhusu vipengele mahsusini vya kimtindo vinavyodhihirika katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Utafiti wake ulichunguza vipengele vya kimtindo katika riwaya hii na jinsi vinavyochangia ukamilifu wake. Vilevile alichunguza namna mwandishi alivyotumia vipengele vya mtindo katika kukuza na kuendeleza ujumbe wake. Utafiti huu ulikuwa na manufaa kwetu kwa kuwa ulituwezesha kuchunguza jinsi mwandishi anavyokuza na kuendeleza ujumbe wake katika riwaya hii. Vilevile ametumia nadharia ya Ufeministi lakini sisi tumetumia nadharia ya uhalisiajabu na pia umuundo.

Mwangi (2013) katika tasnifu yake ya uzamili, alihakiki riwaya za *Babu Alipofufuka* ya S. A. Mohamed na *Watu wa Gehenna* ya Tom Olali akitumia nadharia ya uhalisiajabu. Katika uchunguzi wake amebainisha sifa za kiajabu za wahusika pamoja na matendo yao yanayowafanya waonekane viumbwe wasio wa kawaida. Utafiti huu ulitufaa katika uhakiki wetu katika kuelewa jinsi nadharia ya Uhalisiajabu inavyotumiwa katika uhakiki wa riwaya za kimajaribio.

### **1.9 Njia za Utafiti**

Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani. Katika kufanikisha utafiti huu ilibidi kwanza tusome riwaya husika kwa kina pamoja na vitabu kuhusu nadharia za Uhalisiajabu na Umuundo. Vilevile, tulisoma vitabu anuwai vinavyozungumzia fani kwa ujumla na hasa suala la mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi ambapo tulielekeza

makini yetu. Vilevile tulisoma tahakiki na tasnifu ambazo zinazungumzia kuhusu fani.

Tulitalii kwenye mtandao ili tuone ni mambo yapi yaliyotufaa kuhusu mada yetu. Aidha tulisoma riwaya ya *Mashetani wa Alepo* kwa makini ili tuweze kutambua jinsi mwandishi alivyotumia vipengele anuwai vya fani na hasa mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi kuendeleza ujumbe wake. Tulisoma kuhusu nadharia ya uhalisiajabu na umuundo katika makala na vitabu tofauti tofauti.

Maelezo haya yalikuwa na manufaa kwetu katika kuelewa jinsi nadharia teule zinavyotumiwa katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Baada ya kusoma kwa makini makala na vitabu viliviyotufaa, tulidondo na kuchanganua data zilizotufaa katika utafiti wetu.

### **1.10 Hitimisho**

Katika sura hii tumeelezea mada yetu ya utafiti wetu ambayo ni “Uchunguzi wa vipengele teule vya fani ya *Mashetani wa Alepo*”. Tumedhihirisha tatizo la utafiti, madhumuni pamoja na maswali ya utafiti.

Vilevile, tumeangazia sababu za kuchagua mada ya kazi yetu na tukabainisha upeo na mipaka ya utafiti wetu. Tumetaja misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti wetu ambayo ni umuundo na uhalisiajabu. Tumechangana nadharia hizi kisha tukaelezea waasisi wake na umuhimu wake katika kuihakiki mada yetu. Isitoshe, tumeelezea yaliyoandikwa kuhusu mada yetu kisha tukaelezea umuhimu wake katika somo tunalolishughulikia. Mwishowe, tumbainisha njia ambazo tumezitumia katika utafiti wetu.

## **SURA YA PILI**

### **FANI KATIKA RIWAYA YA *MASHETANI WA ALEPO***

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii tulichunguza vipengele mahsusini vya fani ambavyo ni mandhari, usimulizi na matumizi ya lugha jinsi vilivyotumiwa kuendeleza ujumbe katika kufanikisha *Mashetani wa Alepo*.

Katika kipengele cha mandhari tumeonyesha mandhari ya aina mbalimbali ambamo matukio yanatendeka, yawe ya kihalsia au ya kimazingaombwe. Katika kiambajengo cha usimulizi, tumechanianua hadithi mbalimbali ambazo zimesimuliwa katika riwaya hii na pia tumeonyesha aina mbili za usimulizi zilizotumiwa katika kazi hii. Yaani usimulizi maizi na usimulizi wa nafsi ya kwanza. Pia tumeonyesha umuhimu na udhaifu wa aina hizi za usimulizi. Matumizi ya lugha ni kipengele kingine ambacho tumechunguza kwa kutazama lugha ilivyotumiwa kufanikisha riwaya hii.

#### **2.2 Mandhari**

Wamitila (2008) naye anaielezea istilahi hii ya mandhari kama mahali ambamo matendo yoyote hutokea katika kazi za kifasihi katika wakati maalum. Tunaweza kusema kwamba, mandhari ni ile elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Vilevile anaendelea kusema kwamba, mandhari huathiri sana mkondo wa kimaudhui na huwa na athari kubwa kwenye dhamira kuu katika kazi inayohusika. Mandhari yanaweza kuwa na uhalsia wa kijiografia au yawe

hayana uhalisia wa kijiografia. Pili mandhari huwa muhimu sana kutokana na mchango wake katika kuwapa wahusika wasifu fulani.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa tunaweza kusema kwamba, mandhari ni mahali maalumu palipobuniwa na mtunzi, na mnamatukia matukio mbalimbali ya kazi ya kifasihi. Mandhari hutusaidia kufahamu hisia, tabia, imani na hata maumbile ya wahusika. Mandhari pia hutupa mwelekeo kuhusu maudhui.

Katika *Mashetani wa Alepo*, mandhari ya aina mbalimbali yametumiwa kwa ajili ya malengo tofauti tofauti kwa mfano kutufichulia kuhusu wahusika walivyokaa na kuingiliana katika mazingira wanamoishi. Pia yametuwezesha kung'amua kuhusu mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao. Tunapata mandhari ya aina mbali mbali katika riwaya hii yakiwemo msitu wa Alepo, mito, uwanja wa ndege, hospitali na majengo ya kisasa yakiwa na maabara, chumba cha kulala na hata milima ya taka. Mandhari haya tunayapata kupitia ndoto ya Megido.

### **2.2.1 Chumba cha kulala cha Megido**

Mandhari ya chumba hiki ni ya kihalisia na matukio yanayofanyika hapa ni ya kihalisia na mengine ni ya kiajabu. Katika ukurasa wa kwanza tunaambiwa kwamba, chumba cha Megido kilikuwa kimetiwa nakshi za ajabu. Upande mmoja kulikuwa kumetundikwa ramani kubwa ya kuonyesha sayari mbalimbali yaani dunia, pwagizi, mirihi, zebaki, zuhura, kausi, zohali, vingirizi na mbingizi. Tunaambiwa kwamba kila sayari ilikuwa imetiwa rangi katikati yake. Pwagizi nyeupe, mirihi nyeupe, zohali nyeupe, zote nyeupe, ila dunia ilikuwa na rangi tofauti. Sayari ya dunia ilikuwa nyeusi. Rangi nyeusi ilitiwa katika sayari ya dunia kuashiria giza au maovu

yanayotendeka katika dunia. Rangi nyeupe ilitiwa katikati mwa sayari nyingine ila dunia kuashiria amani na utulivu ulioko katika sayari hizo.

Katika chumba hicho pia tunaona orodha ndefu ya majina ya magonjwa mbalimbali na ugonjwa mmoja umepigiwa mstari kwa wino mwekundu. Katika ukurasa wa pili tunaiona orodha ya magonjwa hayo: malaria, tetekuwanga, saratani, kipukusa, usahafulifu, ukichaa, minyara, mamunyumungi, kimeta, pumu, kinyungi, kichocho, ukimwi na *streptococcus abolo ni pang!* ambao umepigiwa mstari kwa wino mwekundu. Orodha hii ya mangojwa imetumika kama ishara inayotuonyesha magonjwa yanayowatatiza watu katika jamii ya Alepo.

Katika mandhari haya tunapata jambo la kushangaza kwa kuwa tunamwona Megido akiwa katika hali mbili. Yeye ni maiti na pia ye ye yu hai. Ni jambo la kushangaza kwa kuwa katika ulimwengu halisi, mtu hawezi kupatikana katika hali kama hii. Jambo hili linaipatia riwaya hii sifa za kihalisiajabu kwa kuwa mhusika huyu tunamuona akiwa na sifa tofauti na za wahusika halisi. Katika mandhari haya, (uk. 2-7) tunamuona Megido akimtubia *Obong'o Nyakalaga* kutokana na matendo aliyyoyatenda. Anajutia matendo yake hasa lile la kushiriki katika mauaji ya kimbari nchini Alepo.

Anajutia sana kuwaua watu kwa kuwakatakata na kuwateketeza waliojificha kanisani. Katika mandhari haya, tunapata kuyajua baadhi ya mambo aliyyoyatenda Megido katika nchi ya Alepo. Katika (uk.4) Megido anadai kuwa hataki kuwa kama watu wa *Gehenna* hasa baada ya kusoma riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Kimsingi, mandhari haya yanatupatia muhtasari kuhusu maisha ya Megido nchini mwake

Alepo. Mandhari haya vile vile yametufichulia maovu yanayotendeka nchini Alepo kwa mfano mauaji ya kimbari, utengenezaji wa ugonjwa mbaya wa *Streptococcus abolo ni pang!* Uharibifu wa misitu, kuwalawiti watoto kwenye mtandao, kujiingiza katika biashara ya mihadarati na pia kuabudu shetani na pesa.

### **2.2.2 Msitu wa Alepo**

Katika mazingira haya (uk.10) tunaambiwa kwamba, kichwani mwa Megido kulitokea machafu, machafu mwaka wa 3020 – Vision 3020! Machafu haya yalihu mpango wa kuwaangamiza watu wa kabile la Wamaya. Alijiona akiwa na akina Ribit ambao ni watu wa kabile la Wanyakwelekere wakipanga njama ya kuwamaliza wenzao kutoka kabile la Wamaya kutokana na tofauti za kisiasa.

Tunamuona mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* akituibilia dhana mpya ya wakati, kuambatana na sifa za kimajaribio. Hapa, mpaka wa jadi wa sifa ya kiwakati umevunjwa kiasi kwamba matukio yanaacha kuzingatia kanuni za uhalisi wa kiwakati. Kwa mfano anazungumzia kadhia zilizotokea 3020 ilhali kihalisia tunajua katika mapito ya kawaida ya wakati, kipindi hicho hatujakifikia.

Tuanapatiwa sifa za msitu wa Alepo katika ukurasa wa kumi tunapoambiwa kwamba, msitu wa Alepo ulifahamika sana kwa wanyama na ndege wake ainati. Milio ya bundi na wanyama watawalao usiku ilisikika kutoka ndani ya msitu huo. Sifa za msitu huu zinaendelea kudhihirika tunapoelezwa ifuatavyo:

Chura gando na wale wa kiwalo waling'ang'ana kukoroma na chura gando na wale wa kisolo waling'ang'ana kukoroma na chura kigongo wa Ancheta na chura Kigongo wa Maskarini hawakuachwa nyuma ilimradi ilikuwa ni patashika ya sauti mbalimbali za chura. Hizi sauti zilitoka kwa mnyama mmoja chura, lakini hazifahamiki.

Lugha tofauti kiumbe kimoja chura. Chura ni yule yule, sauti ni tofauti lugha ni tofauti. Watapigana kwa sababu ya sauti tofauti walizozitoa.... (uk.11).

Sauti mbali mbali za chura zinaashiria lugha tofauti zizungumzwazo katika nchi ya Alepo. Kwa mfano kuna lugha ya Wamaya na ya Wanyakwerekele. Chura naye ametumiwa kuashiria binadamu. Ingawa watu huongea lugha tofauti tofauti kulingana na makabila yao, wanabakia kuwa binadamu. Wanyakwelekere na Wamaya wanapigana na kuchukiana kwa sababu za kikabila. Tendo hili linatuchorea picha katika ulimwengu halisi ambapo watu huwachukia wenzao kwa sababu za kikabila na chuki ambayo hasa hutokana na tofauti za kisiasa kati ya makabila hayo.

Katika mandhari haya pia tunapatana na mhusika Champion ambaye alikuwa rafiki yake Megido. Katika ukurasa wa kumi na mbili, tunafafanuliwa sifa za mhusika Champion. Tunaambiwa kwamba alikuwa mtu mnene, mrefu na mweusi na kifua chake kipana alikipigapiga kwa majigambo. Aliacha nywele zake kokakuu shaghlabaghala na kumpa sura ya shetani aliyeishi pangoni. Watu walikuwa na shaka na mhusika huyu. Kuna wale waliomwita mnyonya damu na wengine walimwita Champion wa manyoka. Mwendani wake Megido alimhimiza Champion watimize mauaji ya kimbari dhidi ya Wamaya.

Tunaelezewa kwamba, Champion alitazama saa aliyoivalia mkononi ili amhakikishie mwenzake ilikuwa ni wakati upi. Saa ambayo ilikuwa na historia ndefu, saa hii *Chapa Patek Philipe Geneve* ndio ilimfanya apewe jina hili Champion hasa. Alimnyang'anya saa mgeni mmoja mlimbwende aliyeuja kuitembelea Alepo. Tunamwona Champion kama mkatili na mwenye unyama kwa kuwa aliukata mkono wa mgeni huyo kisha akautupa kwenye mto Karuwanga. Mto Karuwanga ni mto

ambao Megido alikuwa akiwalisha ngwena kwa kutumia miili ya watu wa jamii ya Wamaya.

Katika msitu wa Alepo vile vile tunakutana na mhusika Jenerali Pamkwisha ambaye alikuwa ni mzee kutoka jamii ya Wanyakwelekere na alishirikiana na wanasiasa kupanga mauaji ya kimbari dhidi ya Wamaya. Yeye ndiye aliyetayarisha ramani ya kuonyesha zilipokuwa nyumba za jamii ya Wamaya na kutoa majina ya walioishi katika nyumba hizo. Ramani hiyo iliwasaidia Megido na wenzake kutoka kabilia la Wanyakwelekere kuwawinda watu kutoka jamii ya Wamaya.

### **2.2.3 Mandhari ya Maabara ya Eksirei**

Mandhari haya tunayapata katika (uk. 174). Matukio mengi katika mandhari haya ni ya kihalisiajabu. Katika mandhari haya kulikuwa na mukutano wa wajumbe wa ulimwengu na kila mjambe alipewa kazi ya kwenda kutenda maovu kwa watu wa Alepo. Tunaambiwa kwamba vizuu saba vilitumwa katika mukutano huo. Kila kizuu kilikuwa na jitabu la kurasa milioni saba na vilivisoma vijitabu hivyo vyenye anwani ni *Siku Mbaya Kuwa Binadamu* kwa dakika saba. Hili ni jambo la kiajabu kwa kuwa katika ulimwengu halisi hatuwezi kupata jitabu la kurasa kama hizo na pia ni ajabu kuwezekana kusoma jitabu la kurasa milioni saba kwa dakika saba.

Vizuu hivi vilipatiwa majukumu tofauti tofauti kwa mfano, kizuu cha kwanza kilipatiwa kazi ya kuwala wafu. Kizuu hiki kilikuwa cha mtu ambaye katika dunia ya kwanza alikuwa amelaaniwa kutokana na tamaa na ulafi wa mali maishani. Umbo la kizuu hiki lilikuwa la maiti iliyooza na chenye makucha makali na macho yaliyotoa cheche za moto. Mwito wa kizuu hiki ulikuwa kuwafanya wafu wawe

wafu zaidi. Vizuu vingine pia vilikuwa na sura za kushangaza na vilevile vilipewa majukumu ya kufanya kwa mfano kuna kile kiliosha damu ya wafu. Damu ya wanawake waliokufa wakati wa kujifungua. Kizuu kingine kilikuwa na jukumu la kukalia kifua cha wahanga wake na kubadilisha ndoto zao kuwa jinamizi wanapolala.

Kizuu cha saba nacho kilikuwa na jukumu la kuwahami wanyama, misitu na maeneo ya chemichemi za maji. Baadaye vizuu hivyo saba viliungana na kuwa kitu kimoja na vilikuwa na hatima moja ya kuwaua watu wa Alepo waliokosa adabu. Baada ya dakika saba vizuu hivi viliongezeka na kuwa bilioni saba.

Katika mandhari haya ya maabara ya eksirei pia tunaambiwa kwamba, wafu walifufuka na kuja kuwavamia walio hai. Vizuu vilivyokuwa vimefariki kikatili na maumivu mengi mno kwa mfano, kuchomwa kanisani wakiwa hai, kunajisiwa hadi kufariki, kukatakatwa na kutupwa kando ya barabara na kuzikwa kama mbwa. Vilikuwa na hasira nyingi na vilitaka kulipiza kisasi kwa watu walio hai.

Kisa hiki cha vizuu kimetumika kama jazanda inayotuonyesha matendo ambayo hufanyika katika ulimwengu wetu wa kihalisia. Vizuu tunaweza kuvinganisha na wanyonge yaani wasio na nguvu nao walio hai tunaweza kuwalinganisha na mabwanyenye. Kama vizuu hivi vilivyoungana na kuwa kitu kimoja ili viweze kuwaua waliokosa adabu katika nchi ya Alepo, vivyo hivyo katika ulimwengu wa kihalisia wanyonge wanaweza kuungana pamoja na kuwavamia wenye mamlaka ambao ni wakandamizaji ili waweze kupata ukombozi. Watu wanapoungana huwa wanapata nguvu ya kukabiliana na maovu wanayotendewa na mabwanyenye

wakatili ambao hufikiria kwamba hawawezi kutikisika. Ni bayana kwamba, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

#### **2.2.4 Mandhari ya Uwanja wa ndege wa Alepo**

Katika (uk. 190), tunaambiwa kwamba uwanja huu ulikuwa ukiwahudumia takribani watu milioni sabini kwa mwaka. Ndani ya uwanja huu kulikuwa na kichupa chenye virusi vya ugonjwa wa *Streptococcus abolo ni pang!* Watu wengi walipitia karibu na kichupa hicho ingawa walikosa kukikanyanga kichupa hicho inchi chache tu.

Siku moja Obel Sibuth aliyekuwa mfanyakishara kutoka nchi ya magharibi ambamo mlikuwa na umaskini mwingi alipokuwa akienda likizoni kusini mwa taifa jirani la Alepo alikanyanga kichupa hicho kikapasuka na baadaye virusi vilivyokuwa ndani ya kichupa hicho vilianza kuenea na watu wengi walioambukizwa ugonjwa huo. Walioambukizwa walieneza virusi hivyo katika mataifa jirani.

Wagonjwa walipopelekwa hospitalini walianza kuwashambulia manesi na watu wengine na kuwaambukiza ugonjwa huo. Baadaye walioambukizwa walianza kufa na baadaye maiti zao zilianza kuwauma waliokuwa hai. Huu ni uhalisiajabu kwa kuwa katika ulimwengu halisi, wafu hawawezi kuwashambulia watu hai. Mandhari haya yanatufichulia jinsi ugonjwa huo ulivyoenezwa.

Uwanjani huu, biashara nyingi haramu zilifanyika. Kwa mfano pembe za ndovu na dawa za kulevyia zilipitia hapa zikipelekwa Mexico na mataifa mengine. Ufisadi mwingi ulifanyika katika mandhari haya. Kuenea kwa virusi vya *Streptococcus abolo ni pang!* ni jazanda inayotufafanuliwa jinsi ufisadi na uozo wa jamii ulivyoenezwa kutoka nchi moja hadi nyingine.

## **2.2.5 Mandhari ya Mahakamani**

Matukio mengi tunayoyapata katika mandhari haya yalikolea ufisadi mwangi. Kwa mfano, katika ukurasa wa thelathini wa riwaya hii tunaambiwa kwamba, mhusika Fumo alikamatwa zaidi ya mara kumi kwa kushiriki katika biashara ya mihadarati lakini alikuwa akiachiliwa bila kuhukumiwa.

Mahakamani ilikuwa hela zinabadilishana nafasi na haki. Mabwanyenye wengi walikuwa wakishiriki katika biashara za magendo na pindi walipokamatwa walikuwa wakiachiliwa huru baada ya kupatiana mlungura mahakamani. Hata walioshiriki katika mauaji ya kimbari hawakuhukumiwa kwa kuwa walikuwa na ushirikiano na viongozi wakubwa serikalini.

## **2.2.6 Mandhari ya Ndege**

Mandhari haya tunayapata katika ukurasa wa arobaini na moja hadi arobaini na nne. Mandhari haya tunayapata ndani ya ndege ya Boeing 787 Dreamliner ya shirika la ndege la Ethiopia ambayo mhusika Choma aliiabiri. Kupitia mandhari haya, tunapata sifa za mhusika huyu.

Tunaambiwa kwamba yeye alikuwa rafikiye Bw. Taabu na alikuwa meneja wa biashara za Bw. Taabu. Alikuwa ni mwenye kufuja na kuchoma hela. Akiwa mle ndani ya ndege tunamwona kama mpenda anasa kwa kuwa anaagiza vinywaji vyta bei ghali kwa mfano *Glenfiddish Whisky*. Alikutana na mrembo ndani ya ndege hii ambaye alimpatia bahasha iliyokuwa na kijikarakatasi kidogo kilichoandikwa kwa rangi nyekundu swalililomuuliza mhusika Choma alikuwa akiegemea upande upi. Yaani upande wa Wanyakwelekere au Wamaya.

Walipofika nchi ya Alepo abiria wote walishuka na Choma akaenda katika *VIP Lounge* ambapo alikutana na waheshimiwa. Baadaye waliingia katika magari ya kifahari likiwemo Mercedes Benz AMG Vision Gran Turismo ambalo ndilo lilimbeba Choma. Barabarani walihusika katika ajali na *briefcase* iliyokuwa imebebwa na Choma ilichukuliwa na vijana wa kundi la Sisimisi ambalo lilikuwa likiongozwa na Megido. *Briefcase* ile ilitarajiwa kuwa na hela kutoka kwa Bw Taabu ambazo zingetumika kufadhili kundi la Nyuki. Nyuki lilipigania Wamaya na Sisimisi ni kundi ambalo lilipigania Wanyakwelekere. Mandhari haya yanatufichulia sababu ya Choma kusafiri. Alikuwa ametumwa na Bw. Taabu akachukue hela ambazo bwanyenye yeye bwana Taabu alikuwa ameshurutishwa ili kufadhili kundi la vijana haramu. Tunagundua kwamba matajiri walikuwa wakishurutishwa wafadhili makundi haramu. Jambo ambalo lilitimizwa baada ya kuwapatia matajiri vitisho vyaa kuuawa iwapo wangekataa kufadhili vikundi hivyo.

### **2.3 Matumizi ya Lughu na Mbinu Nyinginezo**

Katika sehemu hii, tumejadili maana na mifano ya istilahi kama vile takriri, tashbiha, tanakali sauti, methali na misemo, kuchanganya msimbo na kuhamisha msimbo, chuku, ukiushi wa kisintaksia, tashihisi, maswali ya balagha, nyimbo, taswira, dayalojia, utohozi na matumizi ya maneno ya kigeni.

#### **2.3.1 Takriri**

Watunzi wengi wa kazi za fasihi hutumia mbinu ya takriri kusositiza kimakusudi ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo kama vile mdundo katika fungu la maneno. Takriri huweza kujitokeza katika kiwango cha sentensi au neno.

Mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* ametumia mbinu ya takriri neno hasa katika nyimbo. Mfano wa kuthibitisha haya unapatikana katika wimbo ufuatao:

Sikia mtoto akilia  
Sikia baba akilia  
Sikia mama akilia:

Tena katika wimbo huo huo tunapata;

Mbona mlishiriki  
Mbona mliwachoma  
Mbona mliwakatakata. (uk. 248)

Maneno “sikia” na “mbona” yamerudiwa katika wimbo huu kwa nia ya kutaka kutilia mkazo jambo fulani alilokusudia liifiki hadhira yake. Yaani yametumiwa kusisitiza madhara yaliyotokana na watu kushiriki katika matendo ya kuua. Jambo hili linadhihirika kuitia kifungu kifuatacho:

Simama wewe usiende mbona unaenda? Mbona unaenda kuwaua ndugu zako wa Alepo? Kalausi alisimama. Tena ile sauti kwa nguvu zaidi, “Simama, wewe usiende, mbona unaenda? Mbona unaenda kuwaua ndugu zako wa Alepo?”

Mara nyingine maneno yale yale. Kwa nguvu maradufu. “Simama, wewe usiende, mbona unaenda? Mbona unaenda kuwaua ndugu zako wa Alepo?” (uk.26).

Katika dondo hili, takriri neno “simama” na pia takriri sentensi “mbona unaenda kuwaua ndugu zako wa Alepo” zimetumiwa kutia msisitizo kwa mhusika katika kumkashifu au kumtakaza asiende kufanya mauaji.

Katika ukurasa wa thelathini na tano wa riwaya hii, takriri neno “mpenzi” limetumiwa pale Bi. Shekaina anapomwita mumewe, “Mpenzi! Mpenzi! Mpenzi Taabu.....amka”. Neno “mpenzi” limerudiwarudiwa kuleta hisia kwa msomaji

kwamba Bi. Shekaina alikuwa anamuenzi mumewe kama mpenzi wake. Yaani walikuwa wanapendana mapenzi ya dhati.

### 2.3.2 Tashbihi

Mbatiah (2001) akielezea kuhusu tashbiha anasema kwamba ni tamathali ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Vitu hivyo vinalinganishwa kwa kutumia “kama”, “mithili ya”, na “fanana na”. Katika riwaya hii, kuna matumizi kadha ya tamathali hii ya usemi. Mwandishi ametumia tashbihi ili kuibua dhamira alizodhamiria zimfikie msomaji au hadhira aliposema maneno haya;

Sauti ya Megido ilikuwa na toni mbaya na iliogofya. Sauti ya bundi na yenye sumu kama *Jameson mamba*. Macho makali kama *hajivale* yaliwatazama wenzake (uk.10).

Katika dondo hili, mwandishi ameifananisha sauti ya Megido na sumu ya *Jameson mamba* ili kuonyesha ukali wa sauti ya Megido yaani alikuwa na sauti ya kuamrisha. Ukali wa macho ya Megido umelinganishwa na *hajivale* kumaanisha kwamba macho yalionyesha hatari au dalili ya kutokea kwa vita.

Tamathali hii imetumika konyesha kwamba Megido alikuwa na hamaki kubwa na alikusudia mhusika Ribit ashiriki katika mauaji ya kumaliza watu wa kabila la Wamaya. Mbinu hii pia imetumika kudhihirisha makusudio ya mwandishi. Aidha takiriri imeendelea kutumika katika riwaya hii mwandishi anaposema:

Saa, saa hii ya champion.

Saa hii *Chapa Patek Philippe Geneve* ndio ilimfanya apewe jina hili Champion haswa. Katika uhalifu mwingine wa kimbari, champion aliona saa hii imevaliwa na mgeni mmoja mlimbwende aliyekuja kuitembelea Alepo. Champion alipenda saa hii. Aliona saa hii kama mali ya mohonyo. (uk.13)

Katika dondoo hii takiriri neno “saa” imetumiwa kuweka msisitizo kuwa Champion alipata jina lake kutokana na saa ile *Patek Philipe Geneve* ambayo alimnyang’aya mgeni mlimbwende kwa kuukata mkono uliokuwa umevaliwa saa ile. Uovu ulimfanya awe na sifa ya umaarufu. Mbinu hii vile vile imetumika katika dondoo hili kwa kusudi la kuhifadhi kumbukumbu ya mambo muhimu; kwa minajri ya kutaka kusisitiza jambo fulani.

Katika ukurasa wa ishirini na tisa kuna tashbihi pale tunapoambiwa kwamba mhusika Fumo alikuwa na kovu baya juu ya shavu lake lililomfanya aonekane kama mwenye kulia kila wakati. Tashbihi hapa imetumiwa kutufafanuliwa sifa za mhusika huyu kwamba kila wakati alionekana kama anayelia.

Katika ukurasa wa mia moja ishirini na sita vilevile tashbihi imetumiwa pale tunapoambiwa kwamba, Inspekte Kadara alijigonga ukutani na kuchanika sehemu ya juu ya paji la uso na badaye *damu ilimchuruzika mithili ya bomba*. Tashbihi hapa imetumiwa kutufafanulia kwamba inspekte huyu alikuwa ameumia sana.

### **2.3.3 Tanakali Sauti**

Wasanii wengi wa fasihi hutumia tanakali za sauti katika kazi zao kwa kukusudia kuelezea hisia au kuchora picha ya kutokea kwa jambo fulani. Mbinu hii pia hutumiwa kutia utamu, mvuto na msisimko wa lugha ya mtambaji. Senkoro (1982) anasema kwamba, tanakali sauti ni matumizi ya neno ambalo likitamkwa huelekeea kutoa maana. Matumizi ya tanakali sauti humtia hamu msomaji aendelee kusoma riwaya na kupata ujumbe uliokusudiwa na mtunzi.

Tanakali ya sauti imetumiwa katika riwaya hii pale mwandishi anaposema:

Watu mle kanisani waliziba masikio yao kwa vidole vyao, vichwa vyao vikiwa vimezikwa mikononi mwao. Kazi bure pap, pap, pap, pap. Msichana yule mdogo alilia polepole kwa kwikwi. (uk.259).

Msokile (1992) anasema kwamba, tanakali sauti hujitokeza aghalabu wakati tendo fulani linapotendeka. Mwandishi anatuelezea yale yaliyotokea baada ya sauti ya pap, pap! kutokea kwamba, mtoto alilia kwa kwikwi. Alilia kwa 'kwikwi' ni tanakali sauti iliyotumiwa kuonyesha kwamba majuto yalitokea baada ya sauti 'pap, pap' kusikika. Mwandishi anatumia ujuzi huu kwa nia ya kuishawishi hadhira lengwa iweze kupata ujumbe aliokusudia.

Tanakali zingine zimetumiwa katika riwaya hii kuibua sifa za mandhari mbalimbali kwa mfano katika ukurasa wa hamsini tunaambiwa kwamba, akina Megido walipofika mpaka wa kati yao na Wamaya waliingga kwenye kijumba ambacho kilikuwa na giza totoro na sauti ya 'tik tak tik tak' ndiyo tu iliyokuwa ikisikika. Tanakali ya sauti 'tik tak tik tak' imetumika kutufafanulia kwamba, mandhari yale yalikuwa yametulia sana na sauti hiyo iliwafanya wawe makini chumbani kile kwa kuwa sauti yenyelewa iliwaogofya.

### **2.3.4 Methali na Misemo**

Waandishi wa kazi za fasihi hutumia methali kusisitiza jumbe mbalimbali. Kulingana na Mbatiah (2001), methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha ukweli na busara. Akiendelea kufafanua dhana ya misemo Mbatiah anaelezea kwamba, methali ni sehemu ya turathi za kimapokeo za jamii. Zinabeba falsafa, mila, miko na desturi za jamii.

Kwa hivyo, matumizi ya methali katika kazi za kifasihi hutegemea maana ya misemo hiyo kulingana na jinsi ilivyotumiwa katika mandhari maalum kuibua maana maalumu. Kutokana na haya tunaweza kusema, methali katika utanzu wa fasihi ni mbinu muhimu ambayo mtunzi huitumia kunasa hisia za hadhira lengwa na kuibua vionjo vya kijamii kwa sababu methali hizi hutokana na jamii ambayo mtunzi ameiandikia.

Methali katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo* zimetumika kuanzia sura ya kwanza mpaka mwisho kwa kusudi la kuipamba riwaya yenyewe na kuifanya ivutie wasomaji wake. Kupitia matumizi ya methali, mwandishi ameweza kuwasilisha ujumbe aliokusudia pale anaposema:

Kila mmoja akiapa kuwa wa kwanza kulikata shingo la mwenzake. *Umwaziye arusi hukuwazia matanga* – si kati yao – wao waliwaziana matanga tu. Kila mmoja akiwa ameliteua parange maalum la kulikata shingo la mwenzake. Wote wawili ni wa nchi ya Alepo lakini. (uk.28).

Katika dondo hili methali iliyotumika *umwaziye arusi hukuwazia matanga*, inavuta hisia za msomaji na kumtaka atambue kwamba, mtu yule mnayeishi naye unaweza kufikiria ni rafiki yako kumbe ni adui yako na anaweza kuwa anakuwazia mabaya. Yaani anaweza kuwa na nia ya kukuangamiza.

Methali zimeendelea kutumiwa katika *Mashetani wa Alepo* kushadidia ujumbe. Matumizi ya methali yametegemea uhai wa methali hizo kwa jinsi zilivyotumiwa na hivyo kuleta maana maalum. Misemo na methali katika kazi hii zimetumiwa kunasa hisia za hadhira lengwa. Wasomaji wa kazi hii wakikutana na misemo na methali wanazozifahamu, inakuwa ni rahisi kwao kuelewa ujumbe na ujumbe ambao mwandishi alikusudia uwafikie. Hapa tunapata methali kama:

- a) Kilio huanza wa karibu ndipo wa mbali wakaingia” (uk.53)
- b) “Akaaye karibu na mtoto huandaliwa mwanzo” (uk.106)
- c) “Akomapo mwenyeji na mgeni koma hapo” (uk.109). n.k.

Methali hizi zimetumika kuendeleza dhamira katika kazi hii. Kwa mifano, methali ya kwanza inatufahamisha kwamba maafa yakinke, yule aliyekaribu nawe ndiye anayeweza kuwa na msaada kwako kuliko aliye mbali. Hata hivyo, kuna methali zingine nyingi ambazo zinajitokeza katika riwaya hii na zilitumiwa kuendeleza jumbe mbalimbali. Ifuatayo ni mifano zaidi:

Habari za kuibwa ile *briefcase* zilimfadhaisha mno Makanyaga. Alikwenda mrisi. *Maji yakimwagika hayazoleki.* (uk.45)

Methali hii ina maana kwamba, kitendo kikitendeka kimetendeka na hatuwezi kuyazuia yasitendeke pindi yafanyikapo. Methali zingine ni kama *maji ukiyavulia nguo huna budi kuyaogelea.* (uk.54). Methali hii imetumiwa kuleta maana kwamba, ukijiingiza katika shida fulani huna budi kukabiliana nayo.

### **2.3.5 Kuchanganya Msimbo na Kuhamisha Msimbo**

Maneno ya Kiingereza yametumika katika riwaya hii kwa sababu mbalimbali. Maneno ya Kiingereza ambayo visawe vyake vinaweza kupatikana kwa Kiswahili na mengine ambayo hayana visawe yametumika. Yale yenye visawe yametumiwa na mwandishi kuendeleza msuko wa kimajaribio. Mifano michache ni *business class* (uk.51), *economy class* (uk.50), *suffering* (uk.52), *double secret agent* (uk.51) na kadhalika.

Katika riwaya hii, kuna mawazo mengi ambayo yameelezwa kwa lugha ya Kiingereza. Matumizi ya lugha ya Kiingereza yamesaidia kuleta sifa za kimajaribio

katika riwaya hii. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya matumizi ya lugha ya Kiingereza katika riwaya hii:

*Your brain is filled with illusions  
When your brain visualizes something  
To be fact or fiction, it will be difficult to know the truth  
Little illusions in your brain can lead to wild imaginations  
Do you know visual illusion?  
Truth is in the eye of the beholder. You  
You don't live in the real world  
What you see is interpretation of what your brain interprets.  
You know the causes of mass hysteria?  
Have you read Hoax, myth and manias?  
Your brain is trying to decipher fact from fiction  
The world that you are seeing in your consciousness  
Is not the world that is there?  
Your brain is lying to you  
Your brain is playing trick on you. (uk.81).*

Akilini mwako mmeja mauzamauza na pindi uonapo taswira ya kitu halisi ama cha kufikirika, inakuwa si rahisi kwako kufahamu ukweli. Mawazo yadanganyao ubongo wako yanaweza kukupotosha.

Je, unayafahamu mawazo ya kinjozi? Ukweli ni ule upatikanao kwenye jicho la mtazamaji. Wewe haupo katika ulimwengu halisi. Ukionacho ni tafsiri za ubongo wako. Je unafahamu kinachosababisha hali kubwa ya kushikwa na shetani (pepo) wa kulia au kucheka bila sababu?

Je, umesoma makala yenyenye mzaha, ngano za miungu, mazimwi na pia mashetani? Ubongo unajaribu kufumbua tofauti kati ya ukweli na uwongo. Dunia uionayo nafsini mwako si dunia halisi ila ni akili zako zinakudanganya. Yaani akili yako inakuchezea shere.

(Tafsiri yangu)

Aidha mwandishi ametumia maneno ya Kidholuo maksudi kama vile *Obong'o Nyakalaga* ili kuchimuza hisia fulani. Yaani wale wenye kutenda maovu watahukumiwa na Mungu Muumba ambaye ni *Obong'o Nyakalaga*.

### **2.3.6 Chuku**

Mbatiah (2001) anasema kwamba chuku ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi, aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Katika *Mashetani wa Alepo*, chuku imetumiwa ili kusisitiza kwa kukiuka kaida za matumizi ya lugha zinazodhihirisha ufanisi wa maksudi. Chuku imetumika katika riwaya kueleza sifa za wahusika ambazo zinazua tataruki. Kwa mfano Megido anaelezwa kuwa “mweusi kama usiku wa manane elfu kwa moja”. Mhusika Champion ana sifa za kishetani. Mtunzi anatumia wanyama wanaoogopewa kama vile swila, ngwena na bundi kushadidia hofu.

Katika ukurasa wa arobaini na moja tunaona matumizi ya chuku tunapoambiwa kwamba, kama vile jina nzuri huokoa nayo sura nzuri huokoa. Tunaelezewa kwamba, mhusika Amakelech alikuwa na macho ya gololi na mashimo katika mashavu yake na pindi alipotabasamu ndio sukari ya jicho lenye uhitaji pindi lilipomtazama na kukutana naye akitabasamu. Tunaambiwa waliopendezwa na urembo wa kidosho huyu mionganini mwao alikuwa mhusika Choma. Chuku hapa imetumiwa kuongeza ladha katika riwaya hii na hivyo, kumvutia msomaji aendelee kusoma riwaya yenyewe na bila shaka aweze kupata ujumbe aliokusudiwa na mwandishi. Chuku pia imetumiwa kutuonyesha sifa za mhusika Choma kwamba alikuwa ni mtu mwenye tamaa ya wanawake. Pia tumegundua kwamba, mhusika Amakelech alikuwa na uzuri wa kumtoa nyoka pangoni. Yaani alikuwa kidosho kupindukia.

### **2.3.7 Ukiushi wa Kisintaksia**

Katika *Mashetani wa Alepo*, kuna ukiushi wa kisintaksia.Ukiushi wa kisintaksi unapatikana mwandishi anaposema, “Sehemu nyingine ya ubongo chake kilikuwa hakipo” (uk.213).

Mtunzi pia ametumia maneno ya Kidholuo na mengine ya ajabu kama vile, *Streptococcus abolo ni pang!* Pia kuna mwendelezo wa maneno kwa njia ya ajabu kama vile wxxng.Ukiushi huu umetumiwa kusositiza mambo ya kiajabu katika riwaya hii.

### **2.3.8 Tashihisi**

Wamitila (2003) anaelezea kwamba tashihisi ni pale ambapo kitu kisichokuwa na uhai au uwezo wa kuhisi (urazini au ung’amuzi) wa kibinadamu kinapewa sifa hiyo. Kwa njia hii mvuto wa kisanaa unapatikana.

Aidha hutumiwa ili kuleta athari fulani ya kihisia. Mfano wa tashihisi katika riwaya hii unapatikana katika maneno yafuatayo:

Sauti alianza. Naam, alianza kumhoji Champion.  
Champion aliyekuwa naye-sio vile vingine saba  
vilivyokuwa vinazunguka kama chupa za soda ndani ya  
karakana. Hivyo viliendelea na safari yao isiyokwisha. Ni  
vigumu kujua kilichokuwa kikiendelea. Hata mimi sijui.  
Lakini sauti alijua. Huyu ndiye yule sauti katika riwaya ya  
*Watu wa Gehenna!* (uk.101).

Katika dondo hili, sauti imepewa sifa ya uhai ili kuleta hisia fulani kwa msomaji. *Gehenna* ni motoni na sauti iliyomhoji Champion ilitoka huko motoni ambapo wenye kutenda maovu wanatarajiwa kupelekwa baada ya hukumu. Hisia tunayoipata hapa ni kwamba, Champion atapelekwa motoni baada ya hukumu kuu.

### **2.3.9 Maswali ya Balagha**

Wamitila (2003) anaelezea kwamba maswali ya balagha ni tamathai ya kuulizia maswali ambayo hayahitaji majibu. Huenda maswali haya yasihitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi kwa kila mtu. Katika *Mashetani wa Alepo* maswali ya balagha yametumiwa ili kutilia mkazo. Mifano ya kuthibitisha haya yanapatikana katika dondoo lifuatalo:

Mwenye kuua atauawa-hatimaye  
Na anapouawa, anakwenda wapi? Na kama atafufuka,  
atakuwa nini? Na wale Waliouawa ni hai ama wafu? Mtu  
anaweza kumdhuru aliye hai? Kusema kweli kuna maisha  
baada ya kifo? (uk.47).

Katika dondoo hili, mtunzi ametumia maswali ya balagha ili kusisitiza kuhusu suala la mauaji. Anataka msomaji awaze kuhusu suala la kifo kwa kujiuliza maswali hayo. Maswali ya balagha katika riwaya hii hayajaishia hapo, tunaendelea kuyapata katika kazi hii tunapoelezwa hivi, “Jameni! Mnafikiri hilo ni pango? Isije kuwa mtego wa Wamaya”. (uk.27).

Katika maneno haya, tunakutana na swali la balagha ambalo linatumwiwa kusisitiza kwamba pango waliloliona linaweza kuwa si pango tu, bali ni mtego kwa hivyo walistahili kujitahadharisha.

### **2.3.10 Nyimbo**

Nyimbo nyingi zinajitokeza katika *Mashetani wa Alepo*. Mbinu hii imetumiwa ili kuondoa ukinaifu na kuchimuza maana tofauti. Nyimbo hizi zimetumika kuelezea hisia za binadamu. Matumizi ya nyimbo tunayapata katika riwaya hii. Kwa mfano, kuna wimbo mmoja uliovutia washiriki sana na ulihusu mapenzi.

Laiti, laiti ahee  
Ulimwengu taka  
Laiti, laiti ahee .....  
Wimbo mwingine ulihusu furaha iletwayo na ndoa.

Watu wenda nayo  
Kwao jaha  
Nasi twende nalo  
Kwetu jaha hoyo

Pia mwingine ulihusu umuhimu wa msichana kuwa bikira.

Mwatee, mwatee  
Aliuambia mwenyewe  
Tia mkono upapase ..... (uk.112-119).

Nyimbo hizi zimeelezwa kwa matumizi ya lugha iliyojaa ufundi, umbuji na hisia za hali ya juu. Hisia tunazokumbana nazo katika nyimbo hizi ni za furaha.

Katika ukurasa wa mia mbili arobaini na nane wa riwaya hii, kuna wimbo ambao umetumika kuendeleza maudhui ya hukumu na haki. Katika wimbo huu tunaambiya kwamba, wale wote walioshiriki katika mauaji ya kimbari, walioshiriki katika ghasia za kikabila na pia katika vitendo vingine vya kikatili hawatajiepusha na hukumu. Hata wale waliouawa kikatili na hawakupata haki watalipiza kizazi. Tunaambiya kwamba, waliokufa bado ni hai na watalipiza kisasi. Wimbo huu unaipatia riwaya hii sifa za kimajaribio kwa kuwa katika ulimwengu halisi wafu hawawezi kuwa hai na pia hawawezi kulipiza kisasi. Hata hivyo, umazingaombwe katika wimbo huu umetumika katuonyesha kwamba, waliotenda maovu hawataepuka hukumu kwa vyovyote vile lazima siku moja watahukumiwa.

### **2.3.11 Taswira**

Riwaya hii imeshehenezwa taswira chungu nzima, ambazo bila kufahamu ziashiriavyo, mtu hawezi kuielewa vizuri. Tutaelezea taswira kuu zilizotumika katika

riwaya hii. Mashetani wa Alepo ni taswira ambayo inaashiria wakandamizaji, mabwanyenye na wakoloni mamboleo. Tunaambiwa kwamba nchi ya Alepo ni nchi iliyosheheni uozo wa kila aina. Yaani, ufisadi, mauaji mionganini mwa mengine. Maovu haya yamesababishwa na mabwanyenye ambao wengi wao ni viongozi wa ngazi za juu serikalini.

Wanatumia uongozi wa kimabavu kuwakandamiza wananchi wa kawaida. Ni kutokana na matendo haya duni ambapo viongozi hawa wanajitajirisha kwa mali ya wananchi. Pia wamefanya nchi ya Alepo kuwa jangwa kwa kukata miti kwenye misitu na hivyo, kusababisha hifadhi za chemichemi za maji kukauka. Mashetani hawa vilevile wameshirikiana na wageni kutoka nchi za ng'ambo kushiriki katika biashara ya mihadarati. Vilevile wanashiriki katika biashara haramu ya kusafirisha pembe za ndovu. Wamefanya nchi iliyokuwa na raslimali nyingi, yenyе utulivu na amani nyingi kuwa nchi ya fujo na yenyе umaskini mwangi. Hata kortini, haki haipatikani, wanaopeleka malalamiko yao kuhusu hali mbaya nchini Alepo wanachukuliwa kama maadui na wakandamazaji.

Alepo ina taswira ya nchi inayotawaliwa kimabavu. Kwa mfano, nchi ya Alepo ni nchi iliyokuwa na utajiri wa kila aina. Kulikuwa na wanyama wengi wa mwituni, ndege wa aina mbalimbali warukao angani, mito na hata bahari zenyе maji safi. Watawala wakorofu waliharibu mazingira mazuri yaliyokuwa na hewa safi kwa kukata miti na pia kutia sumu walizozitumia kwenye mashamba yao makubwamakubwa ya maua kwenye mito, bahari na maeneo ya kuhifadhi chemichemi za maji.

Jambo hili lulisababisha wanyama wengi wanaoishi majini kufa na pia kuharibu maeneo ambayo watu wa Alepo walikuwa wakiyapata maji yao ya kunywa. Alepo kwa hivyo ni nchi ambayo imegawanyika mara mbili. Kuna ulimwengu wa matajiri wanaopora mali ya nchi kwa kutumia njia duni kama vile kunyakua mashamba ya wananchi kupitia ufisadi. Viongozi hawa hawayaenzi mazingira ya nchi yao kwa kuwa hata yakiharibika wao hawajali bora watajirike. Ulimwengu wa maskini ni mkubwa katika nchi hii. Wanyonge wanaendelea kuwa wanyonge na matajiri wakandamizaji wanaendelea kutajirika zaidi.

Wanyakwelekere na Wamaya ni taswira nyingine inayoashiria binadamu wa kawaida, wanaonyanyaswa na kudhulumiwa. Hawa ni wananchi wanaotumiwa na matajiri ili kutimiza matakwa yao. Kwa mfano katika nchi ya Alepo, makabila mawili yalikuwa yakinipiganishwa na matajiri waliotaka kuchukua mamlaka nchini. Jambo kama hili hufanyika katika ulimwengu wetu halisi. Kwa mfano nchini Kenya watawala ndio wanaowachochea wanyonge wapigane ili wafaidi wao.

Ndoto nayo ni taswira iliyotumiwa kuashiria kinyume cha uhalisia. Wahusika wengi wanaishi katika ulimwengu wa ndoto. Yaani wamekengeuka. Kwa mfano Megido ni mhusika anayeishi katika ulimwengu wa ndoto kwa sababu ya kuandamwa na maovu aliyoyatendea watu wa Alepo. Yeye anajuta kwa kuwakatakata kwa parange watu wa kabilia la Wamaya na sasa yeye hajui iwapo yu hai ama ni maiti. Haishi katika ulimwengu halisi ila katika ulimwengu wa ndoto.

Simu ya Galaxy S17 ni ishara ya maendeleo ya kimawasiliano. Jambo hili ni kinyume katika ulimwengu wa watu wa nchi ya Alepo kwa kuwa hakuna maendeleo

ya hali ya juu hasa katika uwanja wa mawasiliano. Ni ishara ya utamaduni wa kigeni. Watu wa Alepo wanatumia mawasiliano ya kawaida isipokuwa matajiri ambao ni viongozi waliopora mali ya nchi. Matajiri hawa wanaiga mambo ya kigeni kwa kutumia mali ya wizi huku wananchi wakihangaika.

Mercedez-Benz AMG Vision Gran Turismo ni taswira nyingine inayoashiria hali ya kuneemekewa hapa ulimwenguni. Mabwanyenye waliojitajirisha kwa njia haramu kama kuuza mihadarati wanasafiri kwa magari ya kifahari. Wanajiona kama waliobarikiwa ilhali utajiri wenyewe umeporwa wananchi.

Ngwena nayo ni ishara inayoashiria watu wanaofaidika kutokana na mauaji ya kimbari nchini Alepo. Tunaambiwa kwamba mhusika Champion alikuwa akiwalisha ngwena katika mto Karuwanga na miili ya watu wa Kabilia la Wamaya waliouawa katika vita vya kikabila kati ya Wanyakwelekere na Wamaya. Ngwena hapa imetumiwa kama jazanda inayoashiria wale waliofaidika kutokana na vita vya kimbari. Yaani wanasiasa waovu.

Glinffidish Whisky ni ishara nyingine inayoashiria anasa ambazo asili yake ni nchi za kigeni. Tamaduni za kigeni. Nchini Alepo utamaduni wa kigeni umeingizwa nchini na wale wenye kupora mali ya nchi. Wamepata pesa za kushiriki anasa za aina zozote hapa ulimwenguni. Kwa mfano, tunamwona mhusika Choma akitumia mali ya mwajiri wake bwana Taabu bila kujali. Katika mandhari ya ndege aina ya Boeing 787 ya shirika la ndege la Ethiopia tunamwona mhusika huyu akiitisha kinywaji cha bei ghali ambacho analipia kwa kutumia pesa za mwajiri wake. Jambo hili linaashiria matendo ambayo hutendeka katika ulimwengu wetu wa kila siku. Kwa

mfano wafanyakazi wengi hukosa kuwajibika katika kazi zao. Pia wapo wanaopora mali za waajiri wao bila kujali matokeo.

Wavuvi nao ni ishara ya viongozi wa Afrika, hasa wanaojitajirisha na raslimali za nchi. Yaani wao ni wachumaji. Nchini Alepo, viongozi wa vikundi haramu kama vile kikundi cha Sisimisi na Nyuki wanawapiganisha wananchi na baadaye wanaanza kuchuma mali zao.

Parange nayo ni ishara ya vita. Katika nchi ya Alepo, Wamaya na Wanyakwelekere wanapigana kwa kukatakatana kwa parange baada ya kushawishiwa na viongozi haramu wa kisiasa. Vita hivi vinachangiwa na wanasiasa bandia ambao baadaye wanajineemesha kutokana na vita hivyo. Wao wananyakua mashamba ya wananchi kwa kutumia nguvu na baadaye wanajizalishia mali kutokana na mashamba hayo. Wananchi wanaachwa bila makao na mali yao nyingi inaharibiwa mapigano ya kikabila yanapotokea. Zaidi ya taswira ambazo tumeangazia hapo awali, zipo taswira nyingine zinazoendelea kujitokeza katika riwaya hii.

Taswira ya viongozi inajitokeza tunapowaona wananchi wanyonge wakiahidiwa mambo mengi na viongozi wanaojipendekeza ili wachaguliwe. Wananchi hawa wanapatiwa matumaini makubwa na viongozi hao. Walitarajia kwamba, viongozi waliowachagua wangewaletea maendeleo nchini Alepo lakini badala yake wanazima ari na tamaa ya wananchi wao kwa kufanya mambo kinyume kabisa na matarajio ya wananchi. Wanatunga sheria ambazo zinawakinga wao kutokana na mabaya waliyoyatendea wananchi. Wanashiriki katika ufisadi na kutenda maovu mengi zaidi kama vile kupanga mauaji ya kimbari, kuwachoma watu kanisani na hata kuabudu

shetani. Riwaya hii haijatuacha na pengo kuhusu picha ya viongozi hawa. Imewamulika kabisa na kutupatia picha halisi ya matendo ya viongozi hawa wadhulumiaji.

Taswira ya viongozi dhalimu inajitokeza kupitia viongozi wa makundi haramu kwa mfano Megido ambaye anaongoza kikundi cha *Sisimizi* na pia kupitia mhusika Kalausi aliyeongoza kikundi haramu kijulikanacho kama *Nyuki*. Taswira hii vilevile inajitokeza kupitia Jenerali Pamkwisha na pia kupitia wanasiasa potofu amba walikuwa wakiwadanganya wananchi kwa kuwapa pesa chache ili waweze kuchaguliwa. Viongozi walikuwa wakiongea na wananchi hawa kwa kutumia lugha yenyе ladha iliyoweza kumtoa nyoka pangoni. Walitumia lugha hiyo kuwashawishi wananchi washiriki katika mapigano ya kimbari. Mapigano haya yalikuwa yakiwanufaisha viongozi hawa kisiasa. Pindi walipochaguliwa, viongozi hawa walikuwa hawawayali wananchi waliowachagua ila waliwanyanyasa. Walitumia nguvu za kimabavu kuwatawala wananchi hao. Kupitia taswira riwaya hii inadhihirisha kuwa utumizi wa nguvu katika uongozi ndio chanzo cha taabu nchini Alepo.

Mwisho tunaona taswira ya uhusiano kati ya viongozi na wananchi. Wananchi na watawala wao wametengana kama ardhi na mbingu. Tunaambiwa kwamba, wananchi waliokuwa wakijaribu kutetea haki zao walikuwa wakiuawa kwa kuva viongozi waliwaona kama visiki vilivyowazuia wajineemeshe kifedha kupitia njia za mkato ama magendo. Mahakmani mnyonge hangeweza kupata haki, kwa kuwa fedha zilibadilishana mkono na haki. Viongozi waliohukumiwa kutokana na maovu waliyoyatenda walikuwa wakiachiliwa huru baada ya kutoa hongo. Viongozi hawa

waliwahitaji wananchi nyakati za uchaguzi zilipokaribia tu. Taswira hii inaonyesha wazi jinsi nchi nyingi za ulimwengu wa tatu hukumbwa na tatizo la uongozi mbaya. Uongozi unaosababisha mataifa haya kupata maendeleo duni ndio unaotawala *Mashetani wa Alepo.*

### **2.3.12 Dayalojia**

*Mashetani wa Alepo* imetawaliwa na dayalojia ambazo zimesaidia kuendeleza msuko. Ni kupitia kwa dayalojia baina ya wahusika ambapo tunapata kuendeleza maudhui ya mauaji miongoni mwa maudhui mengine. Katika ukurasa wa mia moja thelathini na tatu, kuna dayalojia kati ya mhusika Fumo na mkuu wa upeletelezi kituoni cha polisi. Katika dayalojia hii, Fumo anahojiwa kuhusu mauaji ya raia na ya polisi. Kupitia dayalojia hii, maudhui ya mauaji yanajitokeza.

Katika ukurasa wa mia moja na arobaini hadi mia moja na arobaini na mbili, kuna dayalojia kati ya Mama na mhusika Magombano. Dayalojia hii inatufafanulia suala la kifo. Wawili hawa wanasema kwamba, binadamu akifa akiwa na gadhabu, ghadhabu hizo hurudi kuwahujumu walio hai hasa waliosababisha hasira kwa mfu huyo kabla ya kufa. Pia kutokana na dayalojia hii tunapata kuelewa kwamba unayemtesa atakutesa. Yaani malipo ya dhambi ni hapa duniani.

### **2.3.13 Ukiushi wa Kimsamiati**

Ukiushi wa kimsamiati katika riwaya hii umejitokeza kupitia kutohoa maneno ya Kiingereza na kuyafanya yaonekane kama maneno ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na Matinde (2012), utohozi ni mbinu ambapo nomino kutoka lugha chanzi hutoholewa na hatimaye hufanyiwa marekebisho kwa kufuata kanuni au sheria za

kifonolojia na kimofolojia za lugha pokezi kabla ya kutumiwa. Pia anasema kwamba, maana ya neno lililotoholewa hubakia ileile ya awali.

Katika *Mashetani wa Alepo*, baadhi ya maneno yametoholewa. Kwa mfano katika ukurasa wa mia moja hamsini na sita tunaona utohozi tunapoelezewa kwamba nchi ya Alepo kwa muda mrefu imejulikana kama nchi ya giza. Nchi ya *madimoni*. *Madimoni*? Neno *madimoni* limetoholewa kutoka kwa jina la Kiingereza *Demons*. Utohozi huu umetumika kuleta hisia kwamba Alepo ilikuwa ni nchi iliyojaa watu wabaya na waovu amba wanalinganishwa na madimoni.

Katika ukurasa wa hamsini na saba vilevile kuna utohozi tunapoambiwa kwamba, Mjombakaka na Nanigwanzula ni wa *spishi* moja licha ya kuonekana tofauti. Wawili hawa walitaka kukwaruzana. Neno *spishi* katika maelezo haya limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza *Species* lenye maana ya viumbwe wa jamii moja. Utohozi umetumiwa hapa kama sitiari inayotuelezea jinsi watu wa jamii moja katika ulimwengu halisi huvurugana na kukwaruzana bila kujali au kukumbuka wao ni kitu kimoja.

Mbinu hii ya utohozi ina ubora na pia udhaifu wake. Kwanza ni mbinu nzuri kwa kuwa ni rahisi kutumiwa katika uundaji wa msamiati. Mnenaji au mzungumzaji yeoyote anaweza kutumia mbinu hii hata bila kuhudhuria mhadhara wowote au kozi yoyote ya isimu. Pili nomino nyingi huweza kuundwa kwa kutumia mbinu hii ili kushughulikia mahitaji ya matumizi katika lugha tofauti tofauti. Hata hivyo, mbinu hii ina udhaifu wake kwa kuwa baadhi ya maneno ambayo hutoholewa kutoka lugha ya Kiingereza, katika lugha ya Kiswahili hutamkwa kwa njia tofauti kabisa. Mbinu

hii vilevile huwalemaza wanajamii katika kuunda msamiati mpya unaoakisi mila na utamaduni wa jamii husika. Zaidi ya mbinu hii kuwa na ubora na udhaifu wake, mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* ameitumia kuwasilisha ujumbe alionua umfikie msomaji.

#### **2.3.14 Matumizi ya Maneno ya Kigeni**

Katika riwaya hii, kuna matumizi ya maneno ya kigeni. Mengi ya maneno hayo yametumika kutoa taswira na hisia mbalimbali. Kwa mfano, maneno ya Kiingereza kama vile *Glenfiddish* katika ukurasa wa thelathini na nane limetumiwa kuashiria anasa za hali ya juu. *Samsung Galaxy S17* ni maneno mengine ambayo yametumika kuonyesha maendeleo ya kimawasiliano katika nchi za kigeni kwa kuwa maendeleo kama hayo hayakupatikana nchini Alepo.

Mwandishi vilevile ametumia maneno ya Kidholuo kwa mfano ametumia neno *Abong'o Nyakalaga* ambalo ni jina la Mungu kulingana na wanajamii wa Wajaluo. Neno hilo limetumiwa kuleta hisia kwamba, Mungu ni mweza yote na atawahukumu wote wenye kutenda maovu.

#### **2.4 Usimulizi**

Sehemu hii itahusu dhana ya usimulizi na mitindo tofauti ya usimulizi. Kulingana na Njogu na Chimerah (2011), usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithini. Pia wanasema kwamba, usimulizi katika ngano huwa ni changamano na huchangia moja kwa moja jinsi ya kueleweka kwa maudhui.

Ijapokuwa usimulizi huwa ni wa kuanzia mwanzo hadi mwisho, yaani wa moja kwa moja, huwa vilevile, unajumuisha mbinu zingine kama vile nyimbo, mahojiano na malumbano, ambazo lengo kuu la kutumiwa ni kuyamulika vizuri zaidi maudhui ya ngano. Hivyo, mbinu hizi zote huwa zinatumwiwa kwa lengo la kuelewaka kwa maudhui kwa mnato zaidi. Ninakubaliana na maelezo ya wataalamu hawa kwa kuwa usimulizi huchangia sana katika uelewekaji wa maudhui katika ngano.

Mlacha (1991) anauelezea usimulizi kama uhusiano uliopo baina ya msimulizi na hadithi yenye. Jinsi msimulizi anavyoingiliana na hadithi na nafasi yake katika uwasilishaji wa hadithi ndiyo hutulekeza kufahamu usimulizi wake. Wamitila (2008) akieleza kuhusu dhana ya usimulizi anasema kwamba, katika kazi yoyote ya kifashihi huwa mna kisa au hadithi fulani ambayo inasimuliwa na msimulizi. Msimulizi huyu husimulia hadithi yake hiyo kwa mtindo fulani na kwa njia maalum.

Usimulizi vile vile unaweza kuangaliwa sambamba na kipengele cha wakati. Kutokana na kipengele cha wakati tunaweza kupata hadithi zilizosimuliwa kwa kutumia wakati uliopita, uliopo na ujao. Hadithi inaweza kutambuliwa imesimuliwa katika wakati uliopita kwa matumizi ya mofu za wakati kama *li*. Zaidi ya hayo, kuna mitindo mingi ya usimulizi ambayo mwandishi anaweza kutumia kuiwasilisha kazi yake. Mitindo hiyo hutofautiana kulingana na jinsi inavyozua athari mbali mbali kwa wasomaji. Kuna baadhi ambayo hutulekeza kumulika hisia zetu kwa msimulizi. Hata hivyo, inamlazimu mwandishi kuteua mbinu bora ya usimulizi atakayoitumia kwa kutegemea yale anayotaka kushadidia katika kazi yake. Msimulizi kwa mfano, anaweza kutumia usimulizi maizi kusimulia hadithi yake.

Msimulizi maizi ni yule awezaye kukielewa kila kitu kinachohusu mandhari, wahusika, hadithi na hata saikolojia ya viumbe wa hadithini. Msimulizi wa aina hii ana uwezo wa kuingia akilini mwa mhusika fulani na kumfafanulia msomaji fikira zinazompitikia mhusika huyo. Msimulizi maizi vile vile hujulikana kama msimulizi mwakote.

Riwaya pia inaweza kusimuliwa kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Mbinu hii ya usimulizi hutofautiana na usimulizi wa nafasi ya tatu kufuatiana na sifa yake ya kutoweza kuyaona yote. Msimulizi apatikanaye katika kazi inayosimuliwa kwa aina hii huwa ana mkabala mmoja wa kipekee. Mawazo anayoyaelezea kuhusu hali, tukio, au mtu huwa ni yake binafsi. Mwandishi vile vile anaweza kumtumia nguli wa hadithi kama msimulizi. Mwisho riwaya au hadithi zipatikanazo katika riwaya zinaweza kusimuliwa kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya tatu.

Mbinu hii ya usimulizi hutofautiana na usimulizi wa nafsi ya kwanza pale ambapo, msimulizi hujikita zaidi katika mhusika mmoja tu. Yale yote anayoyafahamu huwa yanahu su huyu mhusika na haonyeshi kuwaelewa wahusika wake wengine. Mwandishi huwa anatambua tu mawazo, msimamo na mwelekeo wa mhusika huyo mmoja. Mtindo huu wa usimulizi humpatia nafasi mhusika mmoja asimulie hadithi badala hadithi yote isimuliwe na msimulizi mwakote.

#### **2.4.1 Usimulizi Katika Mashetani wa Alepo**

Usimulizi wa *Mashetani wa Alepo* umesheheni hadithi kadha ndani ya hadithi kuu. Hili ni thibitisho kamili kwamba, riwaya hii ni riwaya changamano. Vile vile katika

riwaya hii kuna visaasili. Visa na hadithi hizi zinaipatia riwaya hii sifa za kimajaribio. Tunaangazia baadhi ya hadithi hizo hapa chini.

Riwaya hii inaanza kwa toba ya Megido anapomtibia *Obongo Nyakalaga* kutokana na matendo aliyoyatenda. Anajutia matendo yake hasa lile la kushiriki katika mauaji ya Kimbari nchini Alepo. Anajutia sana kuwauwa kwa kuwakatakata na kuwatekeza watu waliojificha kanisani.

Katika hadithi hii tunapata kuyajua baadhi ya mambo mabaya aliyoyatenda Megido katika nchi ya Alepo. Megido anadai kuwa hataki kuwa kama watu wa Gehenna. Kimsingi hadithi hii inatupa muhtasari wa maisha ya Megido nchini mwake Alepo.

Kuna matumizi ya hurafa pale ambapo mwandishi anazungumzia kuhusu Mjombakaka na Nanigwanzula msituni. Awali hawa wawili walikuwa marafiki wakubwa. Hata hivyo, kuliingia hila wakati mmoja kuhusu uchezaji wa bao. Wafuasi wa mjomba kaka waliongezea mashimo saba juu ya bao ili wakapate ushindi. Na wakati wa mchezo ulipowadia, Mjomba kaka alikiuka kaida za kucheza bao. Hali hii ilizua vita kati ya Mjombakaka na Naningwanzula na kati ya mashabiki wao. Katika mmenyano huo, chura mmoja mbilikimo akaja kuwapatanisha. Hurafa hii ni jazanda ya namna viongozi ambao ni marafiki wao kwa wao wanavyoweza kufarakana wakati wa uchaguzi. Hali hii inapotokea, wanaoumia ni wananchi wa kawaida (mashabiki). Hata hivyo, akija mpatanishi, wanasiasa hawa ambao wamefarakana hukaa wakala pamoja tena.

Kuna hadithi inayomhusu Trevino Morales ambaye ni mlanguzi wa miadarati kutoka nchini Mexico lakini analangua miadarati hiyo hadi Alepo. Yeye ni mmoja

wa wale watu wanaochangia mateso na tafrani zote zinazolikumba taifa la Alepo. Vile vile mwandishi anaitumia hadithi yake ili kuwasaidia wasomaji kuelewa tabia alizokuwa nazo Fumo. Alipenda mauaji ya kikatili na kufanya ufisadi wa kuzuia utekelezwaji wa haki mahakamani.

Vilevile kuna hadithi kumhusu B.W. Taabu ambaye alikuwa tajiri mkubwa. Alishurutishwa kufadhili vitendo vya kihuni vya kundi la kabilia lake la Wamaya. Katika ndoto, anapokea barua na simu za vitisho kutoka kwa Wamaya wenzake kuhusu kufadhili mipango yao ya kuwashambulia Wanyakwelekere. Anajaribu kutoroka lakini anawahiwa na walewale waliomtumia hivyo vitisho. Wanampiga na baada ya siku mbili tangu alipoota ndoto hii, anajipata amekabiliwa na Wamaya kihalisa wakidai hela za ufadhili. Anaishia kumwamuru Choma kumtumia pesa baada ya kumpigia simu akitumia simu yake ya *Samsung Galaxy S17*.

Kwa hivyo, kisa cha ndoto hii ni kama utabiri wa kinachokuja kutendeka. Wakati huo huo, hadithi hii imeweza kutuonyesha hali halisi ilivyokuwa Alepo kwamba, matajiri walishurutishwa kufadhili mauaji ya kikabila ndipo wajiimarishe kisiasa.

Hadithi nyingine ni ile inayomhusu Ulrich Fusako akiwa mbele ya tume ya maridhiano. Anakana kushiriki katika mauaji ya kimbari nchini Alepo. Hata hivyo, analaumiwa na wanachama wa Sisimizi kwa kuwasababisha kushiriki katika mauaji hayo ya Kimbari. Yeye ndiye alikuwa akiyatoa maelekezo ya mauaji. Shahidi wa kwanza alidai Ulrich Fusako hakuua mtu bali alitoa tu maelezo ya namna ya kuyatekeleza. Kwa upande mwingine, Kalausi alitoa ushahidi kuwa hata Urich Fusako aliwaua watu kule Tiwu. Ulrich Fusako anayakana mashtaka hayo yote.

Hadhithi hii inatupa maelezo kuhusu yaliyojiri wakati wa mauaji ya kimbari ya Alepo. Ni nani alitekeleza jukumu lipi?

Kuna hadithi nyingine ya Champion na karakana ile ambapo anawaona watu wakizungushwa kama chupa za mvinyo. Aliwaona watu kama Makanyaga mle karakani. Anajiona mle akiwa mara saba. Kila amri inapotolewa, mhusika mmoja anauawa. Makanyaga anapajaribu kujinusuru, anaanguka shimo lisilo na mwisho. Inaelekea kuwa hadithi hii inaashiria hukumu inayowasubiri wanaoshiriki maovu nchini Alepo na kuwa hakuna namna ya kukwepa hukumu hiyo.

Kuna hadithi kuhusu kwa Nabhany 1897. Hadithi hii inasimulia jinsi watu walivyoishi nyakati za awali kabla ya uhasama kuingia. Inasimulia jinsi watu wanavyosherehekea arusi pamoja na kuishi kwa furaha. Nyakati hizo watu waliishi kwa amani, furaha na umoja. Amina bin Msellem anawaongoza wenzake kusherehekea harusi ya bint Maalim al-Din. Hali hii imebadilika pakubwa ikilinganishwa na nyakati za 3020 ambapo matukio ya mauaji ya kimbari na uhasama wa kikabila unapotekelezwa. Mwandishi anaitumia hadithi hii ili kulinganua walivyoishi watu hapo awali na sasa na kuonyesha kuwa iwapo watu waliishi kwa amani, umoja, haki, ujamaa na upendo miaka ya 1897 basi mbona wasifaulu kufanya hivyo nyakati hizi za 3020?

Fauka ya hayo, mwandishi wa Riwaya ya *Mashetani wa Alepo* anasimulia hadithi kumhusu bwana mmoja aitwaye Chin Tufat kutoka Nchi ya Ha. Chin Tufat alikuwa mfanyabiashara aliyeshiriki ufisadi ulioshamiri katika nchi ya Alepo na kuwa kulikuwa na mtandao mkubwa wa walioshiriki katika ufisadi huo. Ufisadi ni

mojawapo ya matatizo yaliyowakumba watu wa Alepo. Walioshiriki humo walikuwa na moyo wa Kishetani ndiposa walipewa majina ya nyoka. Kwa mfano, Gabon Viper, Forest Cobra, Flat -snouted Wolf snake na kadhalika.

Pia kuna hadithi nyingine inayomhusu samaki, yaani samaki-binadamu aliyeamatwa pwani ya Alepo mnamo April 1, 3017. Baada ya Kukamatwa alisafirishwa hadi Alepo kwa Mv Mashetani. Alichukuliwa baadaye na Chin Tufat. Anadai yeze ni Pandora yule wa Kiyunani.

Anasimulia jinsi Pandora alivyoumbwa na Hephaestus kwa maagizo ya Zeus kama adhabu kwa watu wa ulmwengu wakiwemo watu wa Alepo. Alipewa gudulia dogo ambalo alipolifungua; maovu mengi yalitokea ulmwenguni. Hadithi hii ilisimuliwa na mwenyeji mmoja wa Ziwa.

Pia kuna kisa cha daktari Akila ambaye alikuwa amebeba kichupa kilichokuwa na virusi hatari vya ugonjwa wa *Streptococcus abolo ni pang!* Akiwa katika uwanja wa ndege akidhamiria kusafiri kwenda Tiwu. Hata hivyo, anafia katika uwanja wa ndege kabla ya kusafiri. Kichupa hicho kinachookotwa na mwana wa Sikuzani na kuenda nacho hadi Tiwu ambapo kinapasukia uwanja wa ndege na kuwaambukiza watu wengi hatimaye kuzua hali ya taharuki katika mataifa mbalimbali.

Mwandishi wa *Mashetani wa Alepo* vile vile ametumia visasili katika usimulizi wake kwa madhumuni ya kuendeleza uhalisiajabu. Kwa mfano (uk. 224) ametumia kisasili cha Ghoul. Huyu ni shetani katika visasili vya Kiarabu ambaye hukaa makaburini na kula nyama ya wafu. Katika kusimulia hadithi zake, yaani hadithi kuu na hadithi ndogo ndogo katika riwaya hii, mwandishi ametumia usimulizi wa aina

tofauti. Kwa mfano, ametumia usimulizi mwakote katika baadhi ya sehemu za riwaya na vilevile ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza.

Katika kipengele cha usimulizi tumegundua kwamba, hadithi mbalimbali zilisimuliwa katika riwaya hii vikiwemo visaasili. Jambo hili lilifanya usimulizi wa riwaya uwe changamano. Tumechananua hadithi hizo na pia tukaelezea maana ya kila hadithi. Pia tumeelezea aina mbalimbali za usimulizi zilizotumiwa katika riwaya hii. Yaani usimulizi maizi na usimulizi wa nafsi ya kwanza. Tumegundua kwamba usimulizi wa nafsi ya kwanza ulitumiwa ili kumfanya msimulizi maizi asisimulie kisa chote. Vilevile tuliona umuhimu na udhaifu wa aina hizo za usimulizi.

Usimulizi maizi ndio uliotumika kwa kiwango kikubwa katika riwaya hii. Mfano wa kuthibitisha ni kama ufuatao:

Leo ilikuwa sawa na jana, ambayo ilikuwa sawa na juzi na ambayo ilikuwa sawa na siku kabla ya juzi. Megido hajui kama yuko hai ama ni mfu. Hajui kama yanayotokea ni ndoto ama ni ya kweli. Yeye ni kizuu? Yeye ni maiti? Yeye ni kitu? Mimi sijui. Sijui wanatoka wapi, *nini hasa?* Sijui kama wako, *nini hasa?* Na kama wako, sijui walikuwa vizuu kupidia njia gani. *Nani?* Ninachokijua ni kuwa tuliwatendea visivyo. Ni maiti na wanataka kukufanya wewe msomaji kuwa maiti pia. Umeshuka? Unashtuka kwa nini na *wewe* hukuwatendea maovu? Unasikia kicheko kwa mbali? Watu hufa? Mbona maswali mengi? (uk.2)

Kutokana na dondo hili, tunaona kwamba usimulizi uliotumiwa hapa ni usimulizi maizi. Tunaona kwamba msimulizi ana uwezo wa kujua yale yanayotendeka kichwani mwa mhusika Megido. Katika dondo hili pia tumemuona mwandishi akijipenyeza na kumuuliza msomaji maswali kwa mfano anamuuliza msomaji iwapo ameshtuka? Mwandishi anajipenyeza ili aweze kumweka msomaji katika mawazo yake. Yaani kuelewa kwa mwandishi kuwe sawia na kwa msomaji.

Kupitia usimulizi maizi, mwandishi pia anatumia mbinu rejeshi kwa mfano katika kifungu hiki tunaelezewa kwamba,

Miaka mitano iliyopita, hali haikuwa nzuri sana kwa B.W Taabu kwa kuwa alipoingia ofisini kwake asubuhi hiyo, alikuta barua ya vitisho mezani. (uk.30)

Dondoo hili linaturejesha nyuma miaka mitano na kutufahamisha hali ilivyokuwa kwa mhusika Bw. Taabu.

Mwandishi pia anatumia hadithi za kale katika usimulizi wake. Kwa mfano katika (uk.58) wa riwaya hii, anatusimulia kisa cha kale kinachohusu mjombakaka na nanigwanzula. Ametumia hadithi hizo ili amkumbushe msomaji mambo ya kale na pia aweze kupitisha ujumbe fulani kupitia hadithi hizo.

Usimulizi maizi una umuhimu wake kwa kuwa humwezesha msimulizi kuyaona mambo yote yanayotokea na kwa jinsi hiyo kuyasimulia yote. Hata hivyo, usimulizi wa aina hii kulingana na Wamitila (2008) una udhaifu wake kwa kuwa katika riwaya za kipelelezi, sifa za usimulizi huu za kusimulia kila kitu hubanwa kidogo kutokana na kaida za utanzu wenyewe.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza pia umetumiwa katika riwaya hii. Katika ukurasa wa mia moja sitini na nne, kuna masimulizi yanayohusu samaki binadamu ambapo usimulizi wa nafsi ya kwanza umetumika. Tunasoma:

Tayari nimewaeleza kwamba nilikamatwa eneo la pwani ya Alepo mnamo April 1, 2017 majira ya kama saa saba mchana. Sasa nitawaambia sehemu iliyosalia ya habari yangu. Hiyo siku, chombo kijulikanacho kama MV Mashetani kilikuwa kikifanya safari kuwakamata kamba wadogo. Kama saa sita hivi, wavuvi waliiburuta ile nyavyu na walishangazwa sana kuniona mimi... (uk.164).

Matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza katika dondoo hili ni dhihirisho kamili kuwa hadithi hii imesimuliwa katika nafsi ya kwanza.

Mohamed (1995) anatahadharisha kwamba mtu anayeamu kutumia mbinu hii anastahili kuwa makini sana ili asitumie hizo ‘ni’ na ‘mimi’ kiholela na kwa wingi kiasi cha kuwachosha wasomaji.

## **2.5 Hitimisho**

Katika sura hii, tumechunguza vipengele teule vya fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha na usimulizi. Katika kipengele cha mandhari, tumebainisha mandhari mbalimbali yaliyotumika katika riwaya hii. Pia tumeangalia matukio mbalimbali yanayotokea katika mandhari hayo. Kutokana na mandhari hayo tumegundua kwamba, riwaya hii imechanganya matukio ya kihalisia na kiajabu. Pia tumeng’amua kwamba, matukio mengi katika riwaya hii yanachanganya ndoto na ulimwengu wa kihalisia hivi kwamba, si rahisi kutenganisha matukio ya kinjozi na ya kihalisia. Mandhari mengine ni ya kufikirika na yanatendeka ubongoni mwa mhusika Megido.

Katika kipengele cha matumizi ya lugha, tumeuona ufundi wa lugha ambaou umetumika katika riwaya hii. Kwa mfano, mwandishi anatumia takriri, maswali ya balagha kuchanganya ndimi, misemo na methali mionganoni mwa kunga nyingine alipokuwa anataka kusisitiza jambo fulani. Pia anatumia ufundi huu kutia ladha katika kazi yake na hivyo basi, kumvutia msomaji aweze kusoma riwaya yenewe ndipo aweze kuelewa ujumbe ambaou mwandishi alikusudia umfikie.

## **SURA YA TATU**

### **FANI INAVYOIMARISHA MAUDHUI KATIKA *MASHETANI WA ALEPO***

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tumbainisha ya kwamba katika aina hii ya uandishi fani hutumika kiufundi kuimarisha maudhui. Katika sehemu hii tumeonyesha jinsi maudhui yafuatayo yalivyoimarishwa na fani; dini, uchafuzi wa mazingira, athari za teknolojia, mauaji ya kimbari, dawa za kulevya, ndoa, ujisadi, biashara haramu, siasa na uchumi katika jamii na pia masuala ya jinai. Pia tumeonyesha jinsi vipengele mbalimbali vya fani kama vile, mandhari, nyimbo, methali, na dayalojia vilivyochangia kuwasilisha maudhui mahsusini katika utanzu huu.

#### **3.2 Jinsi Fani Inavyoimarisha Maudhui Katika *Mashetani wa Alepo***

Katika sehemu hii tumeonyesha jinsi fani imetumiwa kuendeleza maudhui katika *Mashetani wa Alepo*.

##### **3.2.1 Maudhui ya Kidini**

Katika *Mashetani wa Alepo*, kuna msisitizo kuwa kuna muumba asiyeonekana ambaye anaangalia matendo ya binadamu na kwamba, atakuja kuyapima kwenye mizani. Mungu huyu ambaye ni muweza wa yote ni *Obongo Nyakalaga*. Katika uk.3, tunaambiwa jinsi uwezo wake unavyotamalaki. ‘*Obongo Nyakalaga*, nisamehe. Nimelia sana. Nataka radhi zako’.

Watakaofikishwa mbele ya haki siku ikifika ni waabudu mashetani ambao wametambulishwa kwa herufi 666. Namba hizi zinawakilisha dini bandia ya

binadamu inayoongozwa na shetani, serikali bandia duniani na mfumo wa kibinafsi wa uchumi wa binadamu unaoendeshwa bila kumtegemea Mungu. Tunapata alama za dini hizi kwenye makanisa yaliyovamiwa na kundi la Megido.

### **3.2.2 Uchafuzi wa Mazingira**

Maudhui haya yanajitokeza katika ukurasa wa mia moja sitini na moja hadi mia moja sitini na nne. Tunaambiwa kwamba Alepo ilijulikana kama nchi ya saratani kwa sababu ya mashetani waliokuwa na tamaa ya pesa. Miji yote ilinuka uchafu na kuzungukwa moshi. Wenye kutafuta mali walifanya kila wawezalo kuchafua hali nzuri ya hewa ya Alepo.

Mashamba makubwa ya maua yalimilikiwa na Mashetani wa Alepo. Sumu iliyotumiwa katika mashamba hayo ilimwagwa katika mito ambayo watu wa Alepo walikuwa wakiitumia kupata maji. Sumu hii ilisababisha sumu ya risasi kuongezeka katika mito hiyo mara saba kuliko jinsi ilivyohitajika.

Tunaelezwa kwamba, maeneo ya chemichemi, mito na hata maji karibu na mji wa Tiwu yalikuwa na rangi ya wekundu wa kutu. Uchafuzi huu wa mazingira ulisababisha wanyama wengi waishio majini kufa. Mandhari ya wakati yametumiwa kuimarisha maudhui haya. Tunaambiwa kwamba, madhara haya yalitokea katika mwaka wa 3011. Jambo hili linatuletea sifa za kimajaribio katika riwaya hii kwa kuwa mwandishi anazungumzia matukio yaliyofanyika katika kipindi ambacho katika ulimwengu halisi hatujakifikia. Hata hivyo, ingawa matukio tunayoyazungumzia yalifanyika katika kipindi cha wakati ambao hatujaufikia, matukio kama hayo hufanyika katika ulimwengu wa kihalisia.

Watu waliofanya juhudini ya kupinga matendo ya uchafuzi wa mazingira waliuawa. Asilimia kubwa ya maji ya mito ya Alepo yalikuwa hayafai kunywewa kwa kuwa yalijaa sumu za kila aina ambazo zilisababisha vifo vingi katika nchi ya Alepo.

Mashetani wa Alepo walikata miti karibu yote katika mlima wa Got Odiero. Matokeo yalikuwa makali. Tufani zilivamia nchi ya Alepo na kuifanya Alepo kukabiliwa na tishio la kuwa jangwa. Serikali ya Alepo ilipojaribu kuweka sheria ya kutokata miti, Mashetani wa Alepo walikataa na kuwahonga maafisa wa misitu. (uk.163).

Kutokana na dondo hili tunaona kwamba, ujisadi ulichangia pakubwa katika uharibifu wa mazingira nchini Alepo. Matendo kama haya hufanyika katika ulimwengu wa kihalisia pale ambapo mabwanyenye hutumia kila njia kujipatia mali. Hata mazingira yakiharibika wao hawajali bora wao watajirike. Wanaotetea haki za binadamu huchukuliwa na mabwanyenye hawa kama maadui kwa kuwa wanapotetea haki zao huwa wanaziba njia ambazo mabwanyenye hao hutumia kupata utajiri wao.

### **3.2.3 Athari Mbaya za Teknolojia**

Athari za kiteknolojia tunazipata katika (uk. 177) ambapo tunakumbana na madhara mbalimbali yanayotokana na teknolojia. Maudhui haya yanaimarishwa na mandhari ya maabara ya eksirei kulikotengenezewa virusi vilivyotumiwa kama silaha. Kwa mfano kulitengenezwa silaha ya kusababisha ugonjwa wa Kimeta, Ukimwi na *Streptococcus abolo ni Pang!*. Magonjwa haya yalikuwa yaambukizwe walio hai na kuwasababishia kifo.

Waliotengeneza virusi hivi walianza kujilinganisha na *Obongo Nyakalaga*. Vivyo hivyo uhandisi wa kibayolojia hufanywa katika maabara zipatikanazo katika

ulimwengu halisi. Magonjwa hutengenezwa kwenye maabara haya na baadaye yanaambukizwa. Ugonjwa wa *Ebola* ni mfano wa magonjwa hayo. Wahandisi hao baadaye hutengeneza dawa za bei ghali ambazo hutumiwa kuwatibu wale walioambukizwa magonjwa hayo. Jambo hili hufanya serikali itumie mali yake nyingi kukabiliana na janga hilo na hivyo kusababisha hasara kubwa katika nchi zilizokumbwa na janga hilo. Wahandisi walitengeneza magonjwa na dawa hizo hutajirika sana.

Kwa njia nyingine teknolojia hizi za uhandisi wa kibayolojia huwafanya watu na nchi zenyenye ujuzi huu kujilinganisha na Mungu kwa kuwa wao wanajiona ni werevu sana na wamemfikia Mungu. Ujuzi huu wa kiteknolojia vilevile tunaweza kuuchukulia kama biashara haramu inayotumiwa kuwanyanyasa wanyonge. Pia tunaweza kuzilinganisha teknolojia hizi na utawala wa kimabavu ambao huwafaidi tu wale wenye mamlaka au nguvu kama tulivyoshuhudia katika riwaya hii.

### **3.2.4 Mauaji ya Kimbari**

Maudhui haya ya mauaji ya kimbari yanajitokeaza katika sehemu nyingi za riwaya hii. Katika ukurasa wa tano kwa mfano, tunaambiwa kwamba ni miaka miwili tangu mauaji ya kimbari yafanyike nchini Alepo. Mauaji haya yalikuwa yakipangwa na wanasiasa kutoka makabila mawili. Kabilia la Wamaya na la Wanyakwelekere. Wanasiasa mashuhuri kama Kalausi na Bwana Taabu waliyafadhili makundi ya vijana yaliyokuwa yakitekeleza mauaji hayo. Kulikuwa na kundi lililojiita Sisimizi na lingine lilijulikana kama Nyuki. Sisimizi lilikuwa la vijana kutoka kabilia la Wanyakwelekere na Nyuki lilikuwa la vijana wa kabilia la Wamaya.

Wanasiasa waliwatumia vijana hawa kufanya mauaji pindi uchaguzi ulipokaribia ili wapunguze watu wa kabilia pinzani na pia wawafurushe watu wa kabilia hilo wasiweze kushiriki katika uchaguzi. Baada ya vita, waliweza kuchaguliwa na watu wa kabilia lao ambalo halikufurushwa na hivyo walipata viti vyta uongozi ambavyo walivitumia kufanya biashara za magendo. Kwa mfano, walifanya biashara haramu ya kuuza pembe za ndovu na mihadarati. Mbali na hayo waliweza kuingiza bidhaa kutoka nchi za kigeni kupitia uwanja wa ndege bila kulipia ushuru. Hali hii ilifanya nchi ya Alepo ikose maendeleo kutokana na ukosefu wa ushuru.

### **3.2.5 Dawa za Kulevyta**

Ulanguzi wa dawa za kulevyta unapatikana katika riwaya hii. Katika (uk.29), dawa za kulevyta zinaingizwa nchini na wageni Trevino Morales na Chin Tufat kwa usaidizi wa maafisa wa Wizara ya Biashara na Viwanda wa Alepo.

### **3.2.6 Ndoa**

Katika *Mashetani wa Alepo*, mwandishi ametumia ndoa kati ya jamii zinazozozana kama daraja ya upatanishi licha ya tofauti ya mila na desturi kati yazo. Katika (uk.8) tunaona kwamba, licha ya Megido kuwa wa jamii ya Wanyakwelekere, anamuoa Siprosa wa jamii ya Wamaya ambayo ilikuwa ikihasamiwa na Megido na wenzake. Ni kupitia mhusika Megido na mke wake Siprosa ambapo maudhui haya yameweza kujitokeza.

### **3.2.7 Ufisadi**

Katika riwaya hii, tunakumbana na wahusika wengi wanaojihusisha na ufisadi. Choma, Jenerali Pamkwisha, Kalausi, Bwana Taabu na Ulrich Fulsako ni mionganoni

mwa wahusika hao. Wahusika hawa wanachangia pakubwa kuimarisha maudhui ya ufisadi. Tunaambiwa kwamba, walijihuisha na ufisadi kwa kuhonga viongozi wakuu wa serikali ili waweze kushiriki katika magendo kama ulangizi wa dawa za kulevyta na uuzaji wa pembe za ndovu. Wahusika hawa wanamiliki mashamba makubwamakubwa na wanaharibu maeneo ya chemichemi za maji kwa kutia sumu walizozitumia katika mashamba yao kwenye mito na kwenye bahari. Jambo hili linasababisha vifo vyta wanyama wengi wa majini. Mabwanyenye hawa Wanaposhtakiwa wanawahonga mahakimu kortini ili wasihukumiwe.

### **3.2.8 Biashara Haramu**

Biashara haramu ni shughuli ya kiuchumi ambayo hufanywa na mtu au kikundi cha watu bila kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa katika jamii. Biashara haramu ni mfano wa biashara ambayo imekatazwa kisheria lakini baadhi ya watu hujihuisha katika biashara hiyo.

Katika *Mashetani wa Alepo*, biashara haramu ilifanya kupitia baharini na pia uwanjani mwa ndege wa Alepo. Bidhaa za magendo zilipitishwa kupitia sehemu hizi. Viongozi wakuu wa serikali na pia viongozi wa vikundi haramu vyta vijana walihuksika na uuzaji wa bidhaa haramu kama miadarati. Pia walishiriki katika biashara haramu ya kusafirisha pembe za ndovu katika miji tofautitofauti ukiwemo mji wa Tiwu.

Katika ukurasa wa mia moja arobaini na nane tunaambiwa kwamba, bidhaa zilizoingizwa nchini Alepo zilitakikana zipitie kwa Mkuu wa Udhibitishaji wa Bidhaa kwa njia ya kieletroniki kutathminiwa na kuchunguza viwango vyta hatari

kwa kila bidhaa ambayo iliingizwa na uamuzi kutolewa kuzuia hali hiyo kupitia huduma za kudhibiti hali zozote za hatari forodhani. Tunaelezewa kwamba, kiinua mgongo kilisababisha bidhaa ghushi na za sumu kuingizwa nchini Alepo. Viongozi wa Alepo waliwakubalia watu wa eksirei kuleta mimea ya sumu nchini Alepo. Ufisadi ulichangia sana uendelezaji wa biashara hii haramu jambo ambalo liliwadunisha wananchi wa Alepo.

### **3.2.9 Siasa na Uchumi Katika Jamii**

Wanasiasa mashuhuri nchini Alepo ndio wanaotawala uchumi. Wanasiisa hawa wanajilimbikizia mali kupidia njia za magendo. Wanaingiza bidhaa hizo nchini bila kulipia ushuru. Hali hii inafanya uchumi wa nchi kuendelea kuzorota. Wanyonge wanaendelea kuwa wanyonge na matajiri wanaendelea kutajirika zaidi.

Wahusika kama vile Travino Morales wanashiriki katika biashara haramu ya kuuza mihadarati kutoka nchi za kigeni kama Mexico. Jambo hili linasababisha uchumi wa nchi ya Alepo kuendelea kuwa duni. Siasa potovu pia zinaifanya Alepo kuwa biwi la kurundika dawa za kulevyia jambo ambalo linachangia kuvuruga biashara za wananchi nchini.

Wahusika kama vile Jenerali Pamkwisha, Kalausi na akina Megido wanashiriki katika mauaji ya kimbari nchini Alepo. Mauaji haya yanavuruga uchumi wa wananchi wa Alepo kwa kuwa mali yao nyingi inaharibiwa wakati wa mapigano haya.

Maudhui haya yanaimarishwa na mandhari ya usafiri ya angani na majini kwa kuwa kupitia vituo hivi, biashara nyingi za magendo zinafanyika. Biashara hizi zinaifanya

nchi ya Alepo ikose ushuru hali ambayo inasababisha uchumi wa nchi kuharibika. Wahusika kama Kalausi, Megido na Jenerali Pamkwisha pia wanachangia kuimarisha maudhui haya wanaposhiriki katika mauaji ya kimbari kama tulivyoona awali. Mauaji haya yanababisha mali nyingi kuharibiwa na hivyo kuufanya uchumi wa Alepo kuanguka.

### **3.2.10 Masuala ya Jinai**

Maudhui haya yamejitokeza katika riwaya hii. Tumethibitisha kwamba, wahusika kama, Ulrich Fusako na Kalausi wametumiwa kuyaendeleza maudhui hayo. Pia mandhari ya msitu wa Tiwu yamechangia maudhui haya. Katika ukurasa wa themanini na tatu hadi themanini na saba wa riwaya hii tunafahamishwa jinsi mauaji yalivyotekelawa. Mmoja wa wanachama wa Sisimizi asiyetambulika anasema kwamba, Ulrich Fusako ndiye aliyekuwa akiwaagiza wanachama wa kikundi hiki kuwateka nyara na kuwaua wakazi wa Tiwu. Katika (uk.83) mtu mmoja anasema kwamba, aliwaua wanaume sabini kwa maelezo ya Ulrich Fusako. Ingawa mtu huyo hakuwahi kushiriki katika mauaji hapo mbeleni, anaelezea jinsi alivyowaua watu wa Tiwu kwa kuwachinja kama mbuzi. Katika (uk.84) mhusika Kalausi anafafanua kwamba, Ulrich Fusako pia alishiriki katika mauaji. Aidha, anasema kwamba Ulrich Fusako aliwaahidi wanachama wa Sisimizi dola elfu saba za Marekani iwapo wangetekelawa mauaji ya watu wa Tiwu.

Kupitia gazeti moja la Alepo *the Aliens* inaelezwa kwamba, watu arobaini na watano waliuawa na wengine kumi wakajeruhwa huko Tiwu. Gazeti hilo lilifanua kwamba, kilichosababisha ugomvi na kisha mauaji ilikuwa ni mgogoro wa ardhi. Katika mandhari ya msitu wa Tiwu, kuna mkutano mkubwa ulioshirikisha watu

walionyang'anywa mashamba yao. Katika (uk. 87), watu hao walitaka serikali iwaondoe wakulima waliovamia mashamba yao la sivyo wachukue sheria mikononi mwao. Kupitia taarifa ya redio katika ukurasa wa themanini na saba tunaambiwa kwamba, watu waliokuwa wamenyang'anywa mashamba yao waliwaua wavamiaji hao kwa kuwachinja kama kuku wakitumia visu vikali. Pia katika ukurasa wa themanini na nane tunaelezwa kwamba, kuna mauaji mengine ya kimbari yaliyofanyika wiki moja iliyopita nchini Alepo.

### **3.3 Mandhari Yanavyoimarisha Maudhui kwa Ujumla**

Kupitia mandhari mbalimbali, maudhui kadha yameendelezwa. Kwa mfano, kupitia mandhari ya chumba cha Megido, maudhui ya magonjwa yanajitokeza katika (uk. 2) Tunaona orodha ya majina ya magonjwa yaliyokuwa yametundikwa ukutani mwa chumba hiki. Magonjwa haya ni taswira inayotuonyesha magonjwa yanayowatatiza watu katika nchi ya Alepo.

Katika mandhari haya vilevile tunakutana na mhusika Megido akitubu dhambi zake. Kwa mfano, katika (uk.3) anaomba msamaha kwa kufanya dhambi kubwa kuliko zote. Yaani dhambi ya kuwakatakata watu wasio wa jamii yake na kunyofoa nyeti zao kwa kutumia parange kali. Pia anaomba msamaha kwa kuwabaka akina mama mabinti zao kwa sababu ya kikabilo.

Kutokana na toba hii, tunapata kuyafahamu maovu mbalimbali yaliyokuwa yakindeka katika jamii ya Alepo. Kwa mfano, tunagundua kwamba, ukabila ulikuwa umeshamiri katika nchi ya Alepo kupitia mhusika Megido aliyejkuwa akiwatendea watu wa kabilia pinzani matendo ya kikatili.

Msitu wa Alepo nao ni mandhari mengine ambayo yanetumika kutufunulia maudhui tofautofauti yanayojitokeza katika riwaya hii. Kwa mfano, maudhui ya ukatili dhidi ya haki za binadamu, mauaji ya kimbari na pia ukabila yanajitokeza kuititia kwa wahusika mbalimbali tunaokumbana nao katika msitu huu. Mhusika Champion kwa mfano, anaonyesha ukatili mkubwa wa kuwauwa watu wa Alepo wasio wa kabilia lake na kisha kuirusha miili yao kwenye mto Karuwanga ambapo wanaliwa na ngwena. Katika mandhari haya vile vile tunapatana na mhusika Jenerali Pamkwisha ambaye anapanga mauaji ya kimbari dhidi ya kabilia la wamaya. Kuititia kwake, maudhui ya mauaji ya kimbari yanajitokeza.

Uwanja wa ndege wa Alepo ni mandhari mengine ambayo kuititia kwayo biashara nyingi haramu zilitendeka. Usafirishaji wa pembe za ndovu na dawa za kulevyu ambao ulikuwa kinyume na sheria za serikali ulifanyika kuititia uwanja huu. Bila shaka maudhui ya biashara haramu tunayaona yakijitozea kuititia mandhari haya.

### **3.4 Nafasi ya Nyimbo katika Uimarishaji wa Maudhui**

Nyimbo ni mbinu iliyotumiwa kwa ustadi mkubwa. Kwanza, nyimbo si rahisi kusahaulika. Pili, ni shuruti la utambaji wa fasihi kwamba wenyewe kusimuliwa wajumuishwe kikamilifu katika kuimba nyimbo zilizomo katika hadithi. Nyimbo hizi aghalabu huwa zinaangazia maudhui ya hadithi moja kwa moja, basi huwa si rahisi kwa mwenye kusoma hadithi kutokumbuka maudhui, hasa pale anapoukariri yeche peke yake, wimbo unaopatikana hadithini. Katika *Mashetani wa Alepo*, nyimbo mbalimbali zimetumika kuendeleza maudhui au jumbe za mwandishi. Kwa mfano kuna wimbo wa ‘walijuta’ unaosema,

Gehenna, Gehenna, Gehenna  
Mahali patakatifu, mahali patakatifu  
Mbona wakija Gehenna wanajuta  
Wajutia nini? Wajutia nini?  
Wakiwa duniani, walishiriki  
Walishiriki mambo mengi  
Na sasa.....  
Wanajuta kukata misitu  
Wanajuta kuwanajisi wasichana  
Wanajuta kuiba dawa za hospitali  
Wanajuta kuchafua mashtakimu na chemichemi za maji  
Wanajuta kueneza ukabila x 3 ..... (uk.6-9)

Kutokana na wimbo huu tunapata ujumbe kwamba, wale walioshiriki katika maovu hapa duniani wanajuta kuwa Gehenna. Gehenna imetumiwa kama jazanda inayotuonyesha kuwa maovu yote yanayotendwa hapa duniani siku moja lazima yatalipiwa. Yaani wenye kuyatenda lazima watajutia siku moja.

Katika ukurasa wa kumi na sita tunaambiwa kwamba, Megido alikuwa mbele ya wale wote na akiwa anaendelea kupiga milundi, aliuimba wimbo. Wimbo wenyewe ulitumika kueneza chuki na ukabila. Alisema kwamba, ye ye ni wa jamii ya Wanyakwelekere na hastahili kulinganishwa na kiongozi wa jamii ya Wamaya kwa kuwa hafanani nao. Katika ukurasa wa sita anasema kwamba, lazima wapigane na jamii ya Wamaya kwa kuwa walichukua ardhi zao. Kupitia wimbo huu, tunakumbana na maudhui ya chuki na ukabila. Kwa hivyo, wimbo hapa umetumiwa kama kiunzi cha kubeba maudhui haya.

### **3.5 Nafasi ya Methali Katika Uimarishaji wa Maudhui**

Methali nyingi katika *Mashetani wa Alepo* zimetumiwa kuwasilisha ujumbe fulani. Jambo hili limewawia rahisi wasomaji kung'amu jumbe mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya hii. Tulipata jumbe hizo kwa kufafanua baadhi ya methali hizo

kulingana na muktadha wa matumizi yake riwayani. Katika ukurasa wa thelathini na tisa kuna methali *ngoja ngoja utampata mwana si wako*. Methali hii imetumiwa baada ya mhusika Choma kumwona na mhudumu wa abiria katika ndege aina ya *Boeing 787 Dreamliner* aliyokuwa akisafiria nayo. Katika ukurasa wa thelathini na tisa tunaambiwa kwamba mhudumu huyo alikuwa kidosho mwenye nywele ndefu zilizofika mpaka katika viwiko vyake. Macho yake ya mviringo yalimfanya Choma ashindwe kutazama runinga iliyokuwa mbele yake. Mhusika huyu anajaribu kila awezalo kufanya urafiki na mrembo huyo. Methali tulioitaja hapo juu imetusaidia kung'amua kwamba, Choma aliwapenda wanawake warembo na hivyo, alikuwa mwenye tamaa na pia mpenda anasa. Maudhui tunayoyapata kupitia methali hii yanahu su tamaa na anasa za ulimwengu.

Katika ukurasa wa ishirini na nane kuna methali *Umwaziye arusi hukuwazia matanga*. Methali hii imetumiwa kuonyesha ukabila na chuki iliyokuwa miongoni mwa watu wa Alepo. Nchini Alepo kulikuwa na vikundi viwili haramu; Sisimizi ambalo liliwapigania Wanyakwelekere na Nyuki ambalo lilipigania Wamaya. Viongozi wa makundi haya walifahamiana sana lakini, kila mtu aliapa kuwa wa kwanza kulikata shingo la mwenzake. Yaani waliwaziana kifo.

Ukurasa wa hamsini na moja pia tunakumbana na methali *Kikulacho ki nguoni mwako*. Methali hii imetumiwa kutufafanulia kwamba mhusika Ulrich Fusako alikuwa msaliti kwa kuwa aliwatumikia viongozi wa makundi yote mawili haramu yaliyokuwa yakipigana lakini viongozi hao wawili walikuwa hawayafahamu hayo. Alikuwa akitoa siri za kundi moja na kuzipeleka kwa kundi pinzani. Kila kiongozi alidhani mhusika huyu alikuwa ni dhahabu kumbe adhabu. Methali tulioitaja hapa

imetusaidia kung'amua kwamba, jirani yako wa karibu anaweza kuwa msaliti kwako.

Katika *Mashetani wa Alepo*, tumesimuliwa kuhusu makabila mawili ambayo yalikuwa yakiishi pamoja kwa amani na upendo, lakini uchaguzi ulipowadia, makabila haya yalikuwa yakigeukiana na kuuana kwa sababu ya tofauti za kikabila na kisiasa. Vivyo hivyo katika ulimwengu wetu watu wa makabila tofautitofauti kwa mfano nchini Kenya, hupigana, huharibiana mali na hata kuuana kwa sababu ya siasa potovu.

### **3.6 Nafasi ya Dayalojia Katika Uimarishaji wa Maudhui**

Kupitia dayalojia, maudhui mbalimbali yameendelezwa katika riwaya hii. Kwa mfano, katika dayalojia kati ya mhusika Fumo na mkuu wa upeletezi kituoni cha polisi uk 133, maudhui ya mauaji yamejitokeza. Kupitia dayalojia hii, sifa za kimajaribio katika riwaya hii zinajitokeza pale ambapo mhusika Fumo anasema kwamba, kilichohusika na mauaji ya raia na polisi ni kama mtu ila lina sura ya kutisha, macho mekundu kama damu, meno marefu, lina nywele ndefu, lina manyoya mwilini na mikono yake ina kucha ndefu kali. Lakini ni kivuli. Aliyehusika na mauaji hayo ameellezewa kupitia uhalisiajabu na ana sifa za kushangaza lakini matendo kama hayo ya mauaji hutendeka katika ulimwengu wetu wa kihalisia na wanaotekeleza mauaji hayo huwa ni binadamu kamili wala si kivuli.

Umazingaombwe katika dayalojia hii umetumika kumulika wale wanaoshiriki katika mauaji ya binadamu wenzao. Wao si kama binadamu, wao ni kama wanyama na hatustahili kuwalinganisha na binadamu halisi.

### **3.7 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeyachanganua maudhui mbalimbali yaliyojitokeza katika riwaya hii. Maudhui yanayojitokeza katika riwaya hii ni kama yafuatayo; maudhui ya kidini, uchafuzi wa mazingira, athari za teknolojia, mauaji ya kimbari, ufisadi na dawa za kulevyta, ndoa kama kiungo cha upatanishi, ufisadi, biashara haramu na pia siasa na uchumi katika jamii. Tumegundua kwamba maudhui mengi katika riwaya hii yanatokana na siasa potovu nchini. Pia tumeonyesha uhusiano ulioko kati ya fani na maudhui katika riwaya hii.

## **SURA YA NNE**

### **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumezungumzia matokeo ya utafiti wetu, hitimisho na mapendekezo. Madhumuni ya utafiti wetu yameafikiwa na maswali yetu ya utafiti yamejibowi. Pia tumetoa mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye.

#### **4.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Tumegundua kwamba, katika riwaya hii kuna matumizi ya mandhari ya aina tofautitofauti ambamo matukio ya aina tofauti yanatokea. Tumeona kwamba, mandhari mengine ni ya kufikirika kwa kuwa yanapatikana akilini mwa wahusika. Kwa mfano, mandhari ya msitu wa Alepo yanapatikana akilini mwa mhusika Megido. Vilevile tumegundua kwamba, katika mandhari haya, matukio ya kiajabu na ya kihalisia yanachanganyikana kwa mfano pale ambapo vizuu vilikuwa vikishambulia wananchi wa Alepo ambao walikuwa wamekosa adabu. Vizuu vilikuwa maiti ilhali wananchi wa Alepo walikuwa watu hai. Matukio mengine katika mandhari hayo yanatokea kupitia ndoto za wahusika na jambo hili linafanya ndoto kuchanganyika na uhalisia. Jambo hili linaipatia riwaya hii sifa ya kimajaribio. Yaani ya kuufanya mpaka kati ya uhalisi na ndoto kuwa mdogo. Labda mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yupo ndotoni.

Kupitia matumizi ya mbinu ya uhalisiajabu, riwaya hii imeweza kumulika uozo wa jamii. Kwa mfano, tumeona watu waliokufa bado wako hai na katika hali tofauti wanaendelea kuathiri maisha ya watu waliohai. Tumeona vizuu vyta waliokufa kwa

njia za kikatili vikiwashambulia na kuwaua wale waliokosa adabu katika nchi ya Alepo. Pia tumeona vizuu vikilinda misitu, wanyama pori na chemichemi za maji zilizokuwa zinaharibiwa na mabwanyenye. Yaani mashetani wa Alepo.

Riwaya hii vilevile imeonyesha ufundi mkubwa wa matumizi ya lugha ambao umeongeza ladha katika riwaya hii. Kwa mfano, kuna matumizi ya methali ambazo zimetusaidia kuelewa jumbe mbalimbali ambazo mwandishi alikusudia kuzipitisha kwa hadhira lengwa. Ufundi huu wa lugha pia umesaidia katika kusisitiza masuala muhimu ambayo mwandishi alikusudia kuyapitisha.

Kupitia usimulizi wa riwaya hii tumeweza kugundua kwamba ubaya na uovu haudumu milele. Tunakumbana na mhusika Megido ambaye anaomba msamaha kwa *Obongo Nyakalaga*. Anasema kwamba, anajutia kwa maovu aliyoyatendea watu wa Alepo. Kuna matumizi ya hurafa na pia visasili katika usimulizi wa visa mbalimbali vyta riwaya hii.

Visasili vimetumiwa kuendeleza uhalisiajabu katika *Mashetani wa Alepo*. Pia kuna hadithi zinazotokea kupitia ndoto. Kwa mfano hadithi ya Bw. Taabu ambaye alikuwa tajiri aliota akishurutishwa afadhili vitendo vyta kihuni vyta kundi la khabila lake la Wamaya. Jambo ambalo baadaye linakuja kujiri katika ulimwengu halisi. Ndoto hapa inatumika kama kionambele cha yale yatakayotendeka baadaye. Jambo hili linaleta sifa ya kimajaribio katika riwaya hii. Katika riwaya za kimajaribio, kuna matumizi mengi ya ndoto na pia matumizi ya vionambele. Jambo hili limedhihirika katika riwaya hii.

#### **4.3 Hitimisho**

Katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo*, fani imetumiwa kwa ufundi mkubwa. Jambo hili limefanya ujumbe ambao mwandishi alitarajia kuwasilisha ueleweke. Fani imetumiwa kutia ladha katika riwaya hii na hivyo kumpatia msomaji msukumo wa kuendelea kusoma.

Vipengele vilivyotumiwa ni pamoja na mandhari. Mandhari ya aina mbalimbali yametumiwa kupitisha ujumbe wa mwandishi na pia kufanikisha kazi nzima. Lugha imetumiwa kwa njia ya ufundi na hivyo ikasaidia kupitisha ujumbe wa mwandishi.

Vilevile tumeona kwamba, matukio yanayozungumzia hayakujihusisha na kipindi kimoja maalum lakini yalihu vipindi vingi. Kwa mfano, tumemwona mwandishi akizungumzia matukio ambayo yalifanyika mwaka wa 1867 na kuyalinganisha na yale yaliyotendeka mwaka wa 3020. Jambo hili linaonyesha kwamba, riwaya za kimajaribio huzungumzia matukio ambayo hutendeka katika nyakati mbalimbali hata zile hatujazifikia. Hii ina maana kuwa riwaya za kimajaribio ni za wakati wote iwe miaka iliyopita, wakati uliopo na wakati ujao.

Usimulizi wa riwaya hii umetuwezesha tugundue kwamba, matukio yanayosimuliwa hayahu su eneo dogo la kijiografia bali yanahu su ulimwengu mzima kwa jumla. Nchi ya Alepo iliyosimuliwa inaweza kuwakilisha nchi zote za ulimwengu kwa kuwa matukio yaliyosimuliwa katika riwaya hii hutendeka katika nchi halisi za kilimwengu.

Maudhui tuliyoyashughulikia yametuwezesha kumulika uozo wa jamii ambao unatendeka katika jamii zetu. Pia tumeona madhara ambayo hutokana na uozo huo

kama uharibifu wa mazingira, mauaji, uenezaji wa magonjwa yanayotengenezewa kwenye maabara. Mwishowe tumengu’amua kwamba, *umwaziaye arusi hukuwazia matanga*. Hili limedhihirika kutokana na vita vya kimbari ambavyo hutekelezwa na wananchi ambao huishi katika nchi moja. Wananchi hao hufanya kazi pamoja lakini ifikapo wakati wa uchaguzi wanashawishiwa wapigane na wanasiasa ambao hutaka kuchukua viti vya uongozi. Mwishowe, vifo vingi hutokea huku wanasiasa bandia wakijinufaisha na harakati hizo za mapigano. Wanasiasa hao tunaweza kuwalinganisha na mbwa mwitu aliyevalia ngozi ya kondoo. Mwisho tumeona kwamba, fani na maudhui yana uhusiano wa moja kwa moja. Tumegundua kwamba maudhui hayawezi kuendelezwa bila ya kuhusisha fani.

Kupitia utafiti huu tumegundua kwamba, riwaya za kimajaribio zina mchango mkubwa sana katika fasihi ya Kiswahili. Kwanza, riwaya hizi hazijifungi katika eneo dogo la kilimwengu bali zinatumiwa kuelezea matukio au mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla. Hii ni kwa sababu katika uandishi wake, mipaka ya kijamii na kimataifa huvunjwa.

Pili, riwaya hizi zinatumika kama kioo cha jamii cha kujitazamia. Kwa mfano, waandishi wa riwaya hizi aghalabu hujenga wahusika wenye nafsi mbili. Mhusika anaweza kuchorwa akiwa mbaya na kisha baadaye anapogueuza nafsi yake kutoka ile ya mwanzo na kuchukua nafsi nyingine, anabadilika na kuwa mtu mwema yaani mwenye maadili mema. Jambo hili linatumika kuonyesha kwamba, ubaya haudumu mtu anaweza kuwa mbaya na baadaye abadili mienendo yake na kuwa mtu mzuri. Wahenga hawakukosea waliponena, mui huwa mwema. Binadamu vilevile anaweza kuwa mtu mzuri kisha awe mtu mbaya.

Hali kama hii hujiri katika ulimwengu wetu wa kawaida pale ambapo wananchi wanaweza kushawishiwa na watu wengine kwa mfano wanasiasa na baadaye wajipate wakifanya maovu. Kwa mfano, wanaweza kushiriki katika mauaji au mapigano ya kimbari ilhali mwanzoni walikuwa watu wema kama tulivyoona katika *Mashetani wa Alepo*. Riwaya za aina hii pia zinatumiwa kuikosoa jamii pale iendapo mrama. Vilevile riwaya hii hutumiwa kama kifungua macho kwa walimwengu ili waweze kujinasua kutokana na minyororo ya uongozi mbaya. Mafunzo mengi kuhusu masuala ya kilimwengu yanazungumziwa kwa kina katika riwaya hizi na hivyo basi, huwapevusha wasomaji kuuelewa ulimwengu kwa ujumla.

Mitindo mipy ya uandishi wa kimajaribio inatumwiwa katika riwaya hizi kuangazia masuala yanayohusu dini, siasa za kilimwengu au kimataifa, filosofia na hata utandawazi. Jambo hili linachangia sana katika kuipa fasihi ya Kiswahili sura mpya hivi kwamba mambo muhimu yanayotendeka katika mataifa yanaweza kuangaliwa kwa undani kwa kutumia mtindo huu mpya wa uandishi kama tulivyoshuhudia katika riwaya ya *Mashetani wa Alepo*.

Kupitia riwaya hii na nyingine kama hii, fasihi ya Kiswahili imepata nafasi ya kuyaangalia matukio ya kijamii kwa namna ya kipekee badala ya kuyatazama kwa njia ya kawaida au iliyozoleka aghalabu katika riwaya sahili. Mtindo wa kihalisiajabu tumeuona ukitumiwa kumulika uozo wa jamii katika *Mashetani wa Alepo* kwa ufanisi mkuu.

#### **4.4 Mapendekezo**

Utafiti wa kuchunguza vipengele teule vyatani unaweza kufanywa kwa kulinganisha au kulinganua riwaya ya *Mashetani wa Alepo* na riwaya nyingine za kimajaribio. Utafiti mwingine unaweza kufanywa katika riwaya hii kwa kutumia nadharia nyingine kutafitia kunga nyingine kwani utafiti wetu umejikita katika mandhari, matumizi ya lugha, usimulizi na pia tumeyachanganua maudhui mbalimbali kisha tukaonyesha uhusiano uliopo kati ya maudhui na fani.

## MAREJELEO

- Bakari, M. (2011). "Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina–Adamu!* (2002) na Mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Barasa, M. (2013). "Vipengele Mahsusи вya Kimtindo Vinavyodhihirika katika Riwaya ya *Watu wa Gehenna*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction: Seeing with a Third Eye*. New York: Routledge.
- Dorsh, T. S. (1965). *Classcial Literary Criticism: Aristotle, Horace, and Longinus*. Harmondworth: Penguin Books.
- Forster, E.M. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin.
- Hawthorn, K. (2001). *Studying the Novel*, 4<sup>th</sup> edition. London: Arnold Publishers.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- \_\_\_\_\_ (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kitsao, J. (1975). "A Stylistic Approach adopted for the Study of Written Swahili Propose Texts." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Magaju, J. (2004). "Uhalisiajabu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ya S. A. Mohamed na *Bina–adamu!* (2002) ya K. W. Wamitila." Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishers.
- Mlacha, A. K. na Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Msokile, M. (1993). *Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

- Mugambi, P. (1982). "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikanya Zilizochapishwa". Tasnifu ya uzamil, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mugwika, F. K. (2012). "Dhana ya Uchimuzi Katika uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya *Mafamba*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose*. Dar es Salaam: IKR.
- Olali, T. (2008). *Mafamba*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- \_\_\_\_\_. (2010). "Structure and Anti-Structure of Swahili Novel: A Stylistic Analysis of *Babu Alipofufuka*" katika The Nairobi Journal of Literature.
- \_\_\_\_\_. (2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- \_\_\_\_\_. (2015). *Mashetani wa Alepo*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Dar es Salaam Press and Publicity Centre.
- Tambasi, P. (2011). "Uhakiki wa Fani Katika *Utenzi wa Tambuka*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- \_\_\_\_\_. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.
- \_\_\_\_\_. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Zamora, P. L. & Faris, B. W. (1995). *Magical Realism: Theory, History and Community*. London: Duke University Press.